


YUKO WAPI, MFALME WA WAYAHUDI?

 Na hakika ninathamini hilo. Hiyo ndiyo zawadi yangu ya kwanza ya Krismasi, kwa hiyo nilishukuru sana. Na, vema, kama naweza tu kuhubiri sasa bila kujaribu kuifungua! Mimi ni kama tu mtoto mwenye matarajio hayo ya Krismasi, a—akisubiri kitu, unajua, unahisi tu kwamba kuna mshangao mdogo na unapaswa kuingia ndani yake. Na, unajua, wakati hata tunapozeeka, sidhani kama tunapoteza utoto wetu wote. Je, unafikiri hivyo? Sisi ni watoto wakubwa tu. Hiyo ni kuhusu hilo.

² Naam, Bwana asifiwe! Tunayo furaha kuwa hapa tena, katika asubuhi hii njema ya Krismasi, tukitazamia baraka za Bwana kuendelea pamoja nasi tunapoendelea katika mkutano, kama nilivyo na hakika Yeye amefanya.

³ Nafikiri, asubuhi ya leo, watakuwa na zawadi kwa ajili ya watoto. Au—au ni...[Ndugu Neville anasema, “Tayari imechukuliwa.”—Mh.] Tayari zimechukuliwa, zawadi za watoto. Naam, hiyo ni nzuri sana.

⁴ Sasa, ningependa tu kutoa ripoti fupi kuhusu mkutano wetu wa mwisho, ikiwa ni sawa, na kwa wakati huu. [Ndugu Neville anasema, “Amina.”—Mh.] Ninyi watu ndio mnaoomba na kumshikilia Mungu, ili mimi niende kwenye ibada hizi. Na ningependa tu kutoa muhtasari kidogo wa—wa mikutano ya mwisho tu.

⁵ Moja ya matukio bora ya mkutano uliopita, ilikuwa katika...kilitokea Shawano, Wisconsin. Ilikuwa kwenye ukumbi wa shule ya upili, jumba jipya la shule ya upili, tulipokuwa karibu tu kuwaombea wagonjwa. Nilikuwa nimetoka tu kufanya wito wa madhabahuni, na wengi walikuwa wameinua mikono yao, kumkubali Kristo kama Mwokozi wao binafsi. Na ndipo ikawa kwamba niliona jambo fulani likitukia, ambalo lilikuwa moja kwa moja kwenye wasikilizaji, mbali kidogo kutoka kwangu. Na alikuwa ni mtu wa karibu miaka sabini ama sabini na mitano. Alianguka akafa, akafa kwa mshtuko wa moyo. Povu likamwagika kutoka kinywani mwake, na maji yakamwagika juu ya nguo zake. Na—na mke wake, akiwa amechanganyikiwa sana, akipangusa uso wake.

⁶ Na—na nilijua hiyo ilikuwa hila ya adui. Yeye anafanya mambo hayo ili tu kuwafadhaisha watu, unaona, na halafu, anapofanya hivyo, inaingia kwenye mshtuko. Imetokea mara nyingi kwenye mkutano. Hivi majuzi tu huko New England ilifanyika hivyo tena, kabla tu ya simu hiyo.

⁷ Na ili kuwazuia watu wasisisimke, mimi... Katika nyakati za aina hiyo, lazima uwe na akili zako, ili kuona kile ambacho Roho Mtakatifu atasema. Kwa sababu, tunafundishwa katika Maandiko, kwamba, “Mambo yote hufanya kazi pamoja kwa wema kwa wale wanaompenda Mungu.”

⁸ Na kulikuwa na watoto wengi wa Mungu, wapenzi Wake. Nami niliendelea kumwangalia yule mtu, nikaona ameshatoka povu kinywani. Na... Na kama mtu yeyote ajuavyo, kifo kinapompata mtu, kwa kawaida maji humtoka, unaona. Na wao... Na mke wake, akipangusa uso wake sana, naye alikuwa akifanya *hivyo* tu. Ili kuwazuia watu wasimtambue, nilisema, “Mumeo, ungetaka mtu ampe maji ya kunywa?” ili kupata usikivu wake.

⁹ Naye akasema, “Ndugu Branham, nakuachia tu yote.” Naye alikuwa m—Mlutheri, kwa madhehebu.

¹⁰ Ndipo nikafikiri ningeita mstari wa maombi, na kuwaleta watu, kuwaombea. Lakini, badala ya kufanya jambo hilo, Roho Mtakatifu akaanza kusogea kwenye mkutano, juu ya watu, kuwaita tu. Na Huyo akapita juu ya yule jamaa mzee, kama mara mbili. Na kisha, ghafla, nikasema, “Tutaomba tu.”

¹¹ Ndipo nilipoanza kuomba, nilijisikia nikiomba, nikaambia kifo hiki, “Mfungue.” Na si zaidi ya ilivyosemwa, hivyo, mpaka mtu huyo aliporudi kwenye uhai tena, na akainuka kwa miguu yake. Na jiji lote likajawa na wasiwasi juu yake, kile Bwana alichofanya.

¹² Na kisha, bila shaka, kwenye mikutano mingine. Na kisa kimoja kidogo ningependa kunukuu, si kuchukua muda wenu mwingi, lakini ilikuwa huko Los Angeles hivi majuzi. Nilikuwa nikiishi na Ndugu Arganbright.

¹³ Na wengi wenu mnajua jinsi ilivyo mahali pale, watu wanapiga simu. Kuna watu walio wahitaji. Hatuwahukumu watu kwa kupiga simu na kutaka maombi. Huo ni wajibu wetu, ni kuwaombea watu hao.

Na ilikuwa mbaya sana pale, kwa sababu tulikuwa na mambo mengi makuu ambayo Bwana Mungu alikuwa amefanya. Na, mmoja, palikuwa na mtu aliyepooza, alikuwa amepooza miaka ishirini na kitu, na amelala kitandani mwake. Na Bwana Mungu akamponya mtu huyo, naye akaja akitembea kutoka mkutanoni. Na hilo lilianzisha mtafaruku mdogo miongoni mwa makanisa.

¹⁴ Kisha, asubuhi moja, nilisikia simu ikilia. Na Ndugu Arganbright, ambaye nilikuwa nikiishi naye, hakuwa ndani tu wakati huo, kuchukua simu. Nami nilichukua simu na kuijibu, na ilikuwa m—mmishenari mdogo wa Meksiko. Naye akasema, “Sikujua kwamba—kwamba ulikuwa mjini, Ndugu Branham.” Akasema, “Ni—ni—ninajua mtakuwa na mkutano usiku wa leo, chini mahali fulani kuelekea Jumba la Ng’ombe.” Naye

akasema, “Nina mvulana mdogo ambaye bado hajafikisha miezi mitano.” Na akasema, “Anakufa, kwa kansa.” Naye akasema, “Najua si kawaida kufanya hivi, lakini,” kasema, “kungeweza kupatikana rehema, kwamba ungekuja na kumwombea huyo mvulana mdogo?” Hebu fikiria, vipi ikiwa huyo alikuwa ni mtoto wako?

¹⁵ Na mimi—mimi nikasema, “Nitamwomba Bw. Arganbright aje kwenye simu, na wewe niambie tu, hebu . . . mwelekeze ilipo hospitali, maana sijui jiji hilo vizuri.” Maili mia nne mraba za jiji; nisingepata hospitali hiyo.

Bw. Arganbright alikuja. Akasema, “Ndugu Branham, wewe . . .”

Nikasema, “Ninajisikia kuongozwa kwa hakika kwamba hii ni ya Roho Mtakatifu.”

¹⁶ Kwa hiyo tulishuka hadi mjini, na pale hospitalini. Na ndugu wa Kimeksiko, ingawa hakuwa mweusi, si mweusi kuliko mimi, na mwanamume wa rika langu hivi. Na mke wake alikuwa mwanamke wa Kifini, maskini mama mwenye nywele zenye rangi ya shaba, mrembo sana. Naye alikuwa muungwana. Na tukaingia hospitalini.

¹⁷ Na, loo, naona vituko vingi, sote tunaona, ambavyo vinatusumbua na kuleta hisia zetu, lakini hicho kilikuwa kimoja cha vibaya zaidi nilivyowahi kuona. Ilibidi wamlete huyo mvulana mdogo . . . karibu na chumba cha muuguzi, na muuguzi maalum. Na, nilipoangalia, kansa ilikuwa imeenea maskini taya zake, hadi sasa, ilibidi wamvike kitambaa kichwani, ili asipasue kichwa chake. Na katika maskini taya zake, ambapo daktari alikuwa amejaribu kuikata kansa, na kutengeneza mitaro mikubwa, huku na huko, namna *hii*, kote kote kwenye koo lake dogo. Na *ilizidisha* tu hiyo kansa, na ningeiita neno hilo, ambalo “lilitawanya” hiyo, neno sahihi lingekuwa. Na ikaingia kwenye maskini ulimi wake, na maskini kinywa cha mtoto, si kipana kuliko *hivi*, maskini ulimi huo ulikuwa umevimba na kutokeza nje yapata umbali *huo*, na ukawa mweusi, na ambao ulifungia hewa ambapo alipumua kutoka puani mwake.

¹⁸ Na huyo baba akatembea huku na huku, kando ya mtoto huyu mchanga, na kusema, “Aloo, Ricky.” Kasema, “Maskini mvulana wa baba! Baba alimleta Ndugu Branham akuombe, Ricky.” Na mtoto mdogo akamtambua baba yake.

¹⁹ Na—na hakuwa na kupumua hata kidogo *hapa* juu, kwa hiyo iliwabidi kukata tundu kwenye koo lake. Kulikuwa na kidogo, ilionekana tu kama filimbi ndogo ya duara ambayo tulikuwa nayo miaka mingi iliyopita, ilikuwa kwenye koo lake dogo. Na alikuwa akivuta pumzi yake kupitia filimbi hiyo. Na muuguzi alilazimika kukaa hapo kila wakati kwa sababu kansa, ikivuja, ingeruhusu . . . kuziba shimo hili dogo. Naye ingemlazimu kuichomoa, namna *hiyo*, mtoko wa kansa

kutoka kwenye hiyo kansa. Na mikono yake midogo ilikuwa imeunganishwa, kwa hiyo hakuweza kushika *hii* kwa mikono yake, ili kuitoa ilipokuwa inamkaba. Na muuguzi huko kila wakati. Alipoanza kukabwa, angefika, achukue vitu na kuvuta uchafu wa kansa kutoka kwenye filimbi yake ndogo pale ambapo unapitia kooni mwake.

²⁰ Na mikono yake midogo, namna *hii*, akijaribu kumshika baba yake, kichwa chake kidogo kimerudi nyuma. Na maskini ninii yake. . . Naam, sisi ni ndugu na dada. Nepi yake ndogo, haikuwa hivyo. . . Mtoto mdogo, kwa ujumla, hakuwa mrefu *hivi*. Bado hajafikisha miezi mitano, na kitu hicho kidogo kilimtambua baba yake! Naye akasema, “Ricky, mvulana mdogo wa baba!” Loo, vipi, kuyeyusha tu moyo wa mtu mgumu. Naye alikuwa akijaribu kucheza naye, ama kumpapasa, namna *hii*.

²¹ Na mimi, nikisimama pale, niliwazia, “Bwana Yesu, ikiwa Wewe ndiwe Chemchemi ya huruma zote, na rehema zote ziko ndani Yako, je, utafurahia kumwona maskini kipenzi hiki amelala hapa, akifa namna hiyo? Siwezi kuamini, na kamwe sitaamini, ya kwamba hayo ni—ya kwamba hayo ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu, kuona jambo kama hilo.” Nikawazia, “Wewe ndiwe Chemchemi ya rehema. Na ikiwa Wewe ndiwe Chemchemi ya rehema, basi Wewe ungewezaje, ungeweza kuwa Mungu wa rehema na kufurahia kuona kitu kama hicho?” Nikawazia, “Ungefanya nini kama ungekuwa umesimama hapa?”

²² Vema, natumai ya kwamba kundi langu dogo hapa linanijua vya kutosha, kujua ya kwamba kama mimi ni mlakole sijui. Ikiwa chochote ninachotaka kuwa, ni mwaminifu. Ninapokutana na Mungu, ninataka kukutana Naye kwa moyo mnyofu, na nimefanya vizuri kadri nijuavyo kufanya.

²³ Lakini Kitu fulani kilizunguma nami niliposema, “Bwana, ungefanya nini Wewe kama ungalikuwa umesimama hapa?” Kitu kilijibu, kikasema, “Nasubiri kuona utafanya nini.”

²⁴ Na nilipokitazama kile kitu kidogo, niliushika mkono wake mdogo wa mtoto, usio mpana kiasi *hicho*, na kuuweka kwenye vidole vyangu, *hivi*, na kuushika. Kisha nikasema, “Kwa imani katika Mungu, ninaweka kati ya hii kansa na mtoto huyu mchanga, Damu ya Bwana Yesu Kristo,” na nikageuka tu na kutoka nje. Baba yake akaja pamoja nami. Sikuweza kusema zaidi.

²⁵ Ndipo nikafika kwenye gari, naye akasema, “Ndugu Branham, hizi hapa zaka kidogo nimekuwa nikikuwekea akiba.”

²⁶ Nikasema, “Loo, ndugu mwenye huruma, usifanye hivyo.” Nikasema, “Hapana. Sichukui pesa.”

²⁷ Kasema, “Lakini hii ni zaka inayoenda kwenye huduma.” Kasema, “Niliweka akiba, nilifikiri ningekuona siku moja.”

28 Nikasema, “Weka kwenye bili ndogo ya Ricky hapo.” Nikasema, “Yeye, atahitaji hiyo.” Na kwa hivyo nikaenda hadi nyumbani.

29 Na ndani ya masaa mawili kutoka wakati huo, taya hizo ndogo zilikuwa zimerudi nyuma, kawaida, ulimi ukarudi chini kinywani mwake. Rehema yenye upendo ya Baba mwenye fadhili na upendo iliona inafaa kumponya mtoto huyo. Asubuhi iliyofuata, mtoto huyo alikuwa anaenda kurudishwa nyumbani, kama mtoto mzima.

30 Na nilipokuwa tu nikijiandaa kuondoka . . . Bila shaka, hiyo ilienea Pwani ya Magharibi. Na hapa daktari fulani maarufu alikuwa amemrudisha mjukuu wake nyuma ya Pasadena, na kuweka kizuizi cha barabarani pale, kumwombea mtoto huyo; ambapo alikuwa amemdunga sindano ya penisilini, ikasababisha kansa kuingia ubavuni mwake, mtoto mchanga, kama miaka miwili.

31 Na kwa hiyo huyu mmishenari mdogo wa Meksiko, akapiga simu, na akasema, “Si—sina budi kumwona Ndugu Branham kabla sijaondoka.” Na mimi na mke wangu tulikuwa tayari kwenye gari.

32 Nami nilikuwa nimevua samaki, miaka michache iliyopita, chini kwenye Mto wa Kutorudi, pamoja na Wafanyabiashara Wakristo. Walt Disney, kundi lile huko nje, walikuwa nayo, mtaalamu wa kurudisha sura ya mnyama, maana ndiyo rekodi ya ulimwengu, ya samaki mdogo aina ya upinde wa mvua. Na nilikuwa nikiirekebisha kwenye gari.

33 Na kulikuwa na ga—gari dogo la abiria na mizigo lilienda juu, nyuma, na kutoka nje akaruka maskini baba huyu wa Kimeksiko. Huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, alipokimbia na kuivua kofia yake; na maskini mke wake wa Kifini. Naye akasema, “Ndugu Branham, hizi hapa zaka ambazo Bwana alikutumia.”

“Loo,” nikasema, “ndugu!”

Kasema, “Unajua, Ricky anaenda nyumbani leo.”

34 Nami nikasema, “Ninashukuru kwa hilo.” Yeye . . . Nilisema, “Lakini nilikuambia uchukue za—zaka na—na kuziweka kwenye bili ya Ricky.”

35 Akasema, “Hilo ndilo tu nililotaka kukuambia juu yake, Ndugu Branham.” Akasema, “Nilipoenda kumlipa daktari, asubuhi ya leo, nilimwekea hizi, pesa hizi. Nikasema, ‘Daktari, nataka kukulipa kiasi kwenye bili.’ Akasema, ‘Bwana, hata usinitajie. Huna deni langu hata kidogo.’ Akasema, ‘Hilo ndilo jambo kuu zaidi ambalo nimewahi kuona likifanyika katika maisha yangu yote.’ Akasema, ‘Hayo ni matukio ya matukio!’ Akasema, ‘Huna deni langu hata senti.’”

³⁶ Inaonyesha tu kwamba Mungu aliye hai angali anaishi. Na sasa kabla hatujafungua Yake . . . Loo, kuna mambo mengi zaidi yametokea. Laiti ningalikuwa na wakati wa kuwasimulia, lakini wakati hautaruhusu.

³⁷ Na sasa, mara tu baada ya mwanzo wa mwaka, Januari, ninaondoka kwenda ng'ambo tena. Kwa ajili ya . . . Nitakuwa Kingston, Jamaika, kwenye—kwenye uwanja wa mashindano ya mbio, kwani mnamo Januari, na kutoka huko kwenda Puerto Rico, na kadhalika.

³⁸ Kwa hiyo hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu, katika maombi, kwa Kristo wetu mkuu, mwenye upendo.

³⁹ Ee Bwana, Wewe umekuwa kimbilio letu katika kila kizazi. Wewe ni msaada uliopo wakati wa taabu. Na kujua ya kwamba Uwepo Wako wenye upendo haushindwi kamwe, hututangulia. Nasi tunafunzwa kuwa Malaika wa Mwenyezi Mungu wamepiga kambi kuwazunguka wale wamchao.

⁴⁰ Utuletee, leo, Bwana, hiyo hofu ya kiungu, tupate kujua ya kwamba sisi ni raia wa mkono Wako, na tutasimama siku moja katika hukumu Yako ya Kiungu. Na kuna dawa moja tu tunayojua, na ambayo Neno Lako linafundisha, hiyo ni Damu ya Mwanao Yesu, anayefanya maombezi kwa ajili yetu, asubuhi ya leo, katika Uwepo wa Mwenyezi, kutuleta katika upatanisho Naye, kwa njia ya wema Wake. Na ndipo tumepewa sisi, neema isiyostahiliwa, nasi tunampenda kwa hili. Na kama sisi . . .

⁴¹ Katika mawazo yetu kuna mamia ya mambo makuu ambayo Wewe umefanya. Na lililo kuu kuliko yote, tunaloweza kufikiria, ni wakati ulipotuokoa kutoka katika maisha ya mauti, ambapo ndani yetu kulikaa kifo kwa sababu ya dhambi na makosa. Lakini kwa kukubali msamaha Wake, kulingana na Neno Lake . . . Kwa maana imeandikwa, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima usiopatikana na mauti.” Nasi tunaliamini, na tumelikubali, na kushuhudia Uwepo wa Roho Mtakatifu.

⁴² Na sasa katika uovu huu wa mwisho, saa za mwisho za historia ya ulimwengu huu, tunakushukuru Wewe, Ee Mungu, kujua hilo; wakati kuna kuchanganyikiwa kwingi kwa akili, “Na watu wanakimbia huku na huko,” kama ulivyosema kwa kinywa cha manabii watakatifu, ya kwamba, siku hii “ungekuja wakati ambapo watu wangetoka Mashariki, kutoka Magharibi, Kaskazini na Kusini, wakitafuta kusikia Neno la kweli la Mungu.” Na tuliishi kuona wakati huo.

⁴³ Na Wewe ulitabiri ya kwamba kungekuwa na wakati, kutoka kusulubishwa Kwako mpaka Kuja Kwako, “Siku ambayo haitakuwa usiku wala mchana. Itakuwa wakati wenye utusitusi, huzuni,” Nuru ya kutosha tu kuona jinsi ya kuzunguka. Lakini ulisema, “Wakati wa jioni, itakuwa Nuru,” Mwana yeye yule, Kristo yeye yule, aliyetokea Mashariki. Na kijiografia, jua

kuvuka sehemu ya usawa ya dunia, na sasa linatua Magharibi, bali ni jua lile lile lililochomoza Mashariki. Vivyo hivyo Mwana wa Mungu yule yule anamtuma Roho Wake katika siku hizi za mwisho, ili kuonyesha kwamba Maandiko Yake hayawezi kuvunjwa, kila Moja lazima litimie.

⁴⁴ Katika mkesho wa Krismasi hii kuu, wakati, hatuna habari bali hii inaweza kuwa ndiyo ya mwisho ya hizi tutakazowahi kuketi pamoja. Na tungeomba kwamba Mwana wa Mungu aliye hai akae katikati yetu asubuhi ya leo, na kutunenea wema Wake na rehema Yake, na atupe msamaha wa dhambi zetu.

⁴⁵ Na tusingependa kusahau, Bwana, wale wanaoteseka na ni wahitaji wa mguso Wako wa uponyaji, Mungu yeye yule aliyemjalila mtoto Ricky kuishi, akawafufua wafu, kama Wewe ulivyoahidi kuwa utafanya katika siku ya mwisho. Nayo Maneno Yako ni kweli. Tunaamini ya kwamba uko hapa asubuhi ya leo, upo kila mahali, na uko tayari hata na zaidi kufanya mengi sana, kuliko yote tunayoweza kuomba au kuwazia. Tunakungoja Wewe, Baba, katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao. Amina.

⁴⁶ Sasa, usiku wa leo, Bwana akipenda, natamani kuwa na ibada ya uinjilisti. Bado sijui kabisa ambapo Ujumbe wangu utakuwa, kwa kuwa mchungaji wetu mpendwa na mwenye fadhili sana ameniomba niwe na ibada hizi mbili leo. Nami nitajaribu hilo, kwa neema ya Mungu. Nami nataka kuzungumza juu ya Masihi ajaye, ama jambo fulani la jambo hilo, kwa ajili ya usiku wa leo, ama kwa njia hiyo.

⁴⁷ Asubuhi ya leo, kwa kuwa ilikuwa ni Kri- . . . Jumapili kabla ya Krismasi, ningependa kuzungumza juu ya jambo ambalo ninaamini watoto wadogo, ambao ndio kwanza waruhusiwe kuondoka na kuchukua nafasi zao kanisani, wangeweza kuelewa; kidogo, kile tungeita, kifungu cha Krismasi.

⁴⁸ Na nyinyi mnaotaka kurejea katika Maandiko matakatifu, mngefungua pamoja nami kwenye Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa pili, tunapolisoma Neno Lake.

⁴⁹ Na msisahau, ibada zitaanza saa moja na nusu. Hiyo ni kweli, sivyo, ndugu? [Ndugu Neville anasema, “Saa moja na nusu. Ndiyo.”—Mh.] Saa moja na nusu, kamili, usiku wa leo. Na itakuwa kama ibada ya saa moja, ibada ya kuhubiri.

⁵⁰ Na sasa ninyi ambao Biblia zenu zimefunguliwa, ningependa tu kusoma kifungu kimoja ama viwili kutoka katika hili, kwa ajili ya fu—fungu, na kuomba ya kwamba Mungu atatupa muktadha.

Sasa Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi katika ninii ya mfalme . . . katika siku za mfalme Herode, tazama, mamaajusi wa mashariki walifika Yerusalemu.

Wakisema, Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.

⁵¹ Lazima walikuwa wamechoka sana. Unaona, a—amri ilikuwa ya dharura. Nayo ilikuwa amri ya mfalme, kwa hiyo haina budi kutimizwa. Na ingeonekana kuwa ya ajabu, kwamba tukio kubwa kama hili tunalolitazama, Krismasi ya kwanza, kwamba amri kama hiyo ingetolewa wakati huo. Lakini, unajua, Mungu wa Mbinguni amechagua tangu awali vitu vyote, kwa njia ya Yesu Kristo, na kwamba kila kitu hakina budi kufanya kazi kulingana na mapenzi Yake makuu. Na walipokuwa wamesimama hapo, upande wa magharibi tu wa Bethlehemu.

⁵² Unapopanda, kutoka chini kwenda Uyahudi, unapanda juu ya mlima, na jangwa la mawe, nchi iliyo ukiwa. Na kutoka katika moja ya barabara kuu za Bethlehemu, kuna njia ndogo inayoenda juu ya mlima, ambayo inaitwa barabara, na si zaidi ya njia ndogo kama tungepata hapa, ambapo wanyama walikanyaga. Kwa sababu, ilikuwa ni njia ya punda, ambapo punda na ngamia hupita, wakishuka kwenda Uyahudi, kutoka Bethlehemu.

⁵³ Na mkiwa mnapanda juu, mkitoka Uyahudi, na kuingia Bethlehemu, na kupasua kilele cha kilima, kuna mwamba mkubwa umewekwa pale, yapata theluthi moja ya ukubwa wa jengo hili. Na lazima ilikuwa karibu huko, ambapo walikuwa wamesimama, baada ya kupanda kilima, kumpa nyumbu mdogo kupumzika. Naye Yusufu alikuwa amechoka sana kwa sababu alikuwa amesukumwa sana siku hiyo, kufika Bethlehemu.

⁵⁴ Kwa sababu, amri ilikuwa imetoka kwa Herode na Kaisari Augusto, kwamba kila mtu lazima arudi mahali alipozaliwa, kulipa kodi. Na kodi daima imekuwa ndiyo uharibifu wa mataifa yote. Kila taifa lililowahi kuanguka, lilianguka kwa kodi zake. Na walikuwa wametozwa kodi.

⁵⁵ Na, loo, ingehitaji mtu mwenye moyo wa chuma, kumfanya mwanamke, katika hali yake, alazimike kutolewa nje ya nyumba na kuenda mbali na nyumba, katika hali yake, kwa sababu unaona ya kwamba alikuwa ajifungue mtoto wakati wowote. Naye alikuwa msichana tu, takriban . . . anaaminika kuwa katika umri wake wa miaka kumi na minane, kumi na tisa. Naye alikuwa ameketi juu ya yule punda mdogo, na yule punda mdogo alipoguna waliposimama kwa pumziko la kitambo tu.

⁵⁶ Naye Yusufu anatembea mpaka ukingoni, kutoka mahali walipokuwa wamesimama, na kutazama chini mpaka Bethlehemu. Ulimwengu haukujua kwamba usiku ule ungeimbwa midomoni mwa watu katika enzi za baadaye! Naye Yusufu, alipotazama na kuutazama mji, na kelele za watu, wengine dhidi ya kulipa kodi zao, na ninaweza kumsikia akisema kitu kama hiki, “Mpendwa, unajua, nina shaka kama

tutapata mahali kwenye hoteli, usiku wa leo, kwa ajili yako. Ninaweza kuwaona watu wakilala barabarani na popote wanapoweza kupata, kulala. Mji umejaa watu. Na mikoa yote karibu, imeingia kwa ajili ya kodi hii.”

⁵⁷ Lakini, ajabu, anapogeuka kwa mshangao, kutazama, mke wake mdogo alionekana kuwa hawezi kujibu. Na wakati anageuza kichwa chake, kuona yaliyompata, aligundua kuwa kulikuwa na mwanga usoni mwake, kwa namna ambayo hakuwa amewahi kuona hapo awali. Na chini ya paji la uso wake mzuri, macho yake yalionekana kuwa yametua juu, akitazama angani, kana kwamba kulikuwa na mwanga wa mbinguni usoni mwake. Naye akageuka na kumgusa kwa mkono.

⁵⁸ Na hatimaye akamtazama, na kusema, “Yusufu, umeona hiyo Nyota ikining’inia kule? Inaonekana kuwa nyota nzuri zaidi ambayo nimewahi kuona katika maisha yangu yote. Inaonekana kuangaza kijiji chote cha Bethlehemu.” Na ninaweza kumsikia akisema, “Tangu jua lilipotua, nimeona Nyota hiyo, Nayo inaonekana kuwa imetufuata.”

⁵⁹ Yusufu, ninaweza kumsikia akisema kitu kama hiki: “Naam, mpenzi, ni—ninaona kitu cha kipekee, kwa maana inaonekana kuwa nyota angavu zaidi katika mbingu zote.” Na kwa kweli hiyo ni kweli.

Yeye ni Nyinyoro la Bondeni, Nyota ya
Asubuhi, (Kama mshairi alivyoiweka.)
Mzuri zaidi ya elfu kumi kwa nafsi yangu.

⁶⁰ Na anaposhika mikono yake, kwa upole, kuzunguka viungo na kiuno cha maskini mpenzi wake, na mke, alimwinua kutoka kwa punda, akampakia, na kumweka chini juu ya mwamba, ili maskini mnyama huyo wa kubeba mizigo apate kupumzika.

⁶¹ Na alipoweka mikono yake kwa upole mabegani mwake, naweza kumsikia akisema kitu kama hiki, “Yusufu, sote tunafahamu kuwa haya yote ni ya ajabu. Hatuwezi tu kuelewa. Lakini, sisi sote wawili tukiwa waamini, tunajua kwamba Yehova ana jambo fulani akiba. Na kwamba ametuchagua sisi; na amenichagua mimi, juu ya wanawake wa dunia hii leo, ili ujumbe huu ufichwe moyoni mwangu.” Unaona, ulimwengu ulifikiri huyo ndiye mtoto wa haramu ambaye angezaliwa, lakini Mariamu alijua ukweli.

⁶² Na, leo, watu wengi wanafikiri jambo lile lile, kwamba, “Watu ambao wamempokea huyu Kristo,” wanafikiri kwamba, “wao ni aina fulani ya mwenye kichaa, au mtu wa sifa mbaya.” Lakini wale ambao wameikumbatia hiyo Roho na Imani hiyo moyoni mwao, wanajua walipo. Hakuna kinachosumbua Hilo.

⁶³ Rafiki yangu mwema alinipigia simu siku chache zilizopita, na alikuwa anazungumza na mtu anayesoma saikolojia na—na a—akili. Na mtu huyu alikuwa amesoma kitabu changu, nao wakasema, “Ikiwa yeye ni mtu wa kiroho, je, unajua kwamba

kuna uzi mmoja mdogo kati ya watu wa kilindi wa kiroho na wendawazimu?” Na mtu huyo alishtuka sana.

⁶⁴ Nikasema, “Usione hiyo kuwa ya ajabu. Bwana wetu aliitwa mwendawazimu. Wanafunzi Wake wote waliitwa wendawazimu. Na wote waliomwabudu waliitwa wendawazimu. ‘Kwa njia inayoitwa uzushi,’ alisema Paulo mashuhuri, ‘ndivyo ninavyomuabudu, Mungu wa baba zangu.’” Wao si wendawazimu. Lakini, ulimwengu, kuhubiriwa kwa Injili ni upumbavu kwa wale wanaoangamia. Lakini ilimpendeza Mungu, kupitia upumbavu huu, kuwaokoa wale watakaoamini.

⁶⁵ Na wakati wao, maskini hawa mume na mke, wakiketi pale na kutazama nje ng’ambo ya bonde hilo, na kuona hii Nyota kuu ikiangaza Mashariki; mbali, mamia ya maili mbali na hapo, kule nyuma kuvuka milima, na bahari, kule India, kulikuwako na Mamajusi wakitazama pia.

⁶⁶ Sasa, mamajusi hawa tunaowazungumzia, waliitwa . . . Wao kweli ni Mamajusi, ambao ni wanajimu wanaotazama nyota. Waliitwa, basi, “watu wenye busara.” Na wangelipo hata wa leo. Nimezungumza nao, mara nyingi. Na mara zote hutembea watatu-watatu, kwa sababu hao watatu hawana budi kukubaliana. Na tatu ni uthibitisho. Na huko India, hivi majuzi, ningewaona wameketi barabarani, wamekusanyika pamoja, wamevaa sawa kabisa na Mamajusi hawa wa kwanza. Hawabadiliki.

⁶⁷ Nao ni waabudu wa Mungu mmoja wa kweli. Wao ni watoto wa Ibrahimu, kupitia mke mwingine. Nao wanaamini kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli. Ni mara ngapi nimewaona makasisi wa Kiislamu wakipiga kengele kubwa namna *hiyo*, na kupiga mayowe, “Kuna Mungu mmoja wa kweli na aliye hai, na Muhammad ni nabii Wake.”

⁶⁸ Tunasema, “Kuna Mungu mmoja wa kweli na aliye hai, na Yesu ni Mwanawe.”

Nao wanasema, “Na iwe mbali na Mungu kuwa na Mwana!”

⁶⁹ Nilijaliwa kuona karibu watu laki moja wakija kwa Kristo, kwa wakati mmoja, kwa sababu ya Uwepo Wake na yale aliyofanya huko India.

⁷⁰ Sasa, Wahindi, ambao tunawaita mamajusi, walikuwa wa kwanza, katika Biblia, wakiwakilishwa kama Waamedini na Waajemi. Utaipata katika mlango wa pili wa Danieli. Hiyo, hiyo ndiyo sababu mmishenari anasema, “Ni vigumu sana kumgeuza Mwislamu kutoka kwenye imani yake, kwa Ukristo kwa sababu wanatoka kwa Waamedini na Waajemi wa kale ambao sheria zao hazibadiliki wala hazivunjiki. Wengi wenu ninyi wasomaji wa Biblia mnajua jambo hilo, Waamedini na Waajemi, kwamba hawakubadili sheria zao. Wakati kitu, tangazo lilipotolewa, lilidumu milele. Kwa hiyo wakati Mwislamu anapojitenga na

kuelekea Ukristo, kila kitu kimekufa kwake, kwa sababu amevunja sheria zao.

⁷¹ Na watu hawa, walimngojea Mungu mmoja wa kweli, na wanamwabudu katika mwanga wa moto mtakatifu. Nao wangepokea kuzunguka mioto hii na kumngojea Bwana. Na wengi wao walikuwa na vyumba vya uchunguzi, kitu kama tulicho nacho leo, na wangependa kwenye sehemu hizi juu sana milimani, na wangetazama kila msogeo wa nyota. Wanadai, kwamba, “Kabla Mungu hajafanya jambo lolote duniani, Yeye daima hulionyesha mbinguni kwanza.” Na wako sawa.

⁷² Daima, Mungu hulionyesha kwa ishara za mbinguni, kwanza. Tangu lini Yeye aliwahi kufanya jambo lolote ambalo hakuonyesha ishara ya mbinguni, kwanza? Wazia jambo hilo, katika kila wakati unaotaka, na Mungu daima huonyesha ishara mbinguni, kwanza, kabla hajafanya lolote duniani. Huja kutoka katika mambo ya kimbinguni, huanguka ndani ya maumbile, na kudhihirishwa; kila wakati, kila wakati.

⁷³ Na hivyo wakati huu haukuwa tofauti. Na wale Mamajusi walikuwa wakitazama zile sayari za mbinguni zinazoonekana, nyota, miezi, na kila kitu ambacho wangepokea kuona kwa macho yao. Nao walijua kila nafasi, mahali ambapo kila nyota huketi. Walijua kalenda hiyo ya wanajimu vile vile tunavyojua Maandiko. Na kama kitu kimoja kidogo kimeharibika, wanakijua, kwa kuwa ni ishara. Nao walikuwa wakiangalia ishara hizo, kwa makini, kila saa ya usiku. Waliitazama. Si ajabu kwamba Mgeni akitokea angani angewafanya wote wasumbuke! Si ajabu Mgeni akawatikisa, kidogo! Kwa sababu, walijua kila moja ya nyota hizo, nao walizichunguza, kisayansi, na kutoka katika kila hatua.

⁷⁴ Na wangepokusanyika kuuzunguka moto huu. Nao waliuwasha kwa mafuta matakati, nao ukawaka, nao wangepokea mle ndani, kwa sababu waliamini, kwamba, “Mungu alikuwa ni Moto ulao.” Na ndivyo Yeye alivyo.

⁷⁵ Unaona, katika Matendo, mlango wa 10 na kifungu cha 35, Maandiko yanasema ya kwamba, “Mungu hapendelei mtu, lakini Yeye huwapokea watu wowote watakaomcha na kumheshimu, bila kujali wao ni nani.” Hao ni ninyi Wamethodisti, na Wabaptisti, na Wapresbiteri, Walutheri, ama—ama Wakatoliki, ama chochote ulicho. Kama wewe ni mwaminifu moyoni mwako, Mungu atakupata nafasi, kukuleta katika Nuru ya Kiungu ya rehema Yake. Yeye ni Mungu, Naye amewajibika kupitia ahadi Yake. Basi ni juu yako, kile utakachofanya baada ya kuipokea; basi unaweza kustahimili hukumu. Lakini hadi wakati huo, huwajibiki, unatembea katika yote unayojua.

⁷⁶ Basi hawa Mamajusi, nao walikuwa wakikwea, baada ya kuabudu kuzunguka mahali patakati, pa moto, huku ukiwaka,

na kuangalia ndani ya miale yake mitakatifu, na kustaajabu kama uvuvio wa Mungu huyo ambaye alikuwa ni Moto ulao... “Uwepo Wake, dunia itaangamia.” Alipoangalia hilo, basi angepata uvuvio wake. Kisha angeingia kwenye mnara, na angetazama huku na huko, ili kuona kama kitu chochote kilikuwa kimesonga. Nao walifanya hivi, mwaka baada ya mwaka, siku baada ya siku, saa baada ya saa, milenia baada ya milenia. Walitazama nyota, miili. Na walikuwa wakitoa magombo na wangeyasoma.

⁷⁷ Na hapana shaka ilikuwa katika usiku huu fulani, kwamba walikuwa wakijadiliana kuhusu ku—kuanguka kwa himaya na kuanguka kwa falme, na jinsi ambavyo kwamba ulimwengu ulikuwa umeinuka kuingia mahali fulani na kuanguka tena, na kadhalika, kwamba kulikuwa na gombo lililotolewa. Na hapana shaka kilikuwa ni Kitabu cha Danieli. Nao walikuwa wakijadiliana jambo fulani pale, ambalo Danieli alisema, “Kungekuwa na Jiwe lililochongwa kutoka mlimani, bila kazi ya mikono.”

⁷⁸ Na lazima ilikuwa wakati walipokuwa wakifikiria juu ya hili, huku mioto mitakatifu ikiwaka, ambapo walitokea kuona kwamba kulikuwa na Mgeni kati yao, jambo ambalo hawakuweza kuelezea. Hakuna lolote la magombo yao lililosimulia habari Zake. Hakuna maandishi yao yaliyosema lolote kuihusu, bali ilikuwa ni Hiyo hapo! Hawangeweza kulikana. Walitazama sayari za juu, nao walijua ya kwamba kitu fulani cha kimbinguni kilikuwa kimetukia.

⁷⁹ Oh, Yeye ni mzuri sana! Yeye atavutia usikivu wa kila mtu ambaye amemkusudia Uzima, labda katika njia zao wenyewe za kuabudu. Lakini Yeye ni Mungu, na Yeye anaijua mioyo ya watu, na Yeye anawaangalia, na Yeye anawalinda, na Yeye anawafikisha mahali! “Kilindi kinapoita Kilindi,” lazima kuwe na Kilindi kuitikia wito huo. Kama mtu ana kiu ya kitu fulani, inaonyesha ya kwamba kuna Kitu huko nje cha kuitikia, kuzima hiyo kiu.

⁸⁰ Kama ambavyo nimesema mara nyingi: kabla ya kuwa na pezi kwenye mgongo wa samaki, kulikuwa na maji kwanza kwa ajili yake kuogelea, au asingekuwa na pezi ya kuogelea. Kabla ya kuwa na mti wa kukua ardhini, lazima kuwe na ardhi, kwanza, la sivyo hakungekuwa na mti.

⁸¹ Miaka kadhaa iliyopita, nilipokuwa nikiisoma, niliona katika makala gazetini, ambapo mvulana mdogo alikula vifutio kutoka kwenye penseli shuleni. Na siku moja mama yake alimkuta nje kwenye ukumbi wa nyuma, akila pedali ya baiskeli yake. Naye alishangaa ni nini shida ya kijana huyo mdogo. Alimpeleka kliniki, kwa uchunguzi. Walipouchunguza maskini mwili wake, madaktari waligundua kwamba alihitaji salfa. Nayo salfa iko kwenye mpira. Kwa hiyo, kabla ya kuweza kuwa

na hamu katika mfumo wake, kwa ajili ya salfa, ilibidi kuwe na salfa kuitikia shauku hiyo, la sivyo hangekuwa na shauku hiyo kamwe.

⁸² Na kabla ya kuwa na kiumbe, inabidi kuwe na Muumba wa kuumba kiumbe hicho.

⁸³ Ni mwanamume au mwanamke gani hapa ndani leo, mvulana au msichana, ambaye hana shauku ya uzima? Niambie mwanadamu, leo hii, ambaye hataki uzima, kuishi milele, nami nitakuonyesha mwendawazimu asiyejua, kwa maana hakuna lililo kuu kuliko uhai.

⁸⁴ Je, ungetoa nini leo, ikiwa ungemiliki dunia na bidhaa zake zote? Ungeitoa kwa fahari, kuishi milele, na kuwa maskini. Uzima! Ni wangapi wenu nyinyi wazee mngetoa kila kitu mlichio nacho, ili kurudi kuwa mvulana au msichana tena? Kila mtu anautafuta. Kwa nini? Uko mahali fulani, la sivyo usingeonea shauku.

Nyinyi watu wagonjwa mko hapa ndani kwa sababu gani, leo, kama nyinyi ni wagonjwa? Mnatafuta nini? Ni nini kinachowafanya mje kwa maombi? Kwa sababu kuna kitu ndani yako! Haidhuru wewe ni mfuasi wa kanisa gani, umetiwa chapa gani, hiyo haina uhusiano wowote nayo. Wewe ni binadamu. Wewe ni kiumbe cha Mungu. Na kuna Kitu fulani ndani yako, kinachokuvuta kuelekea mahali fulani. Na kwa hakika kama kulivyo na mvuto moyoni mwako, baada ya daktari labda kukukatia tamaa, ya kwamba bado kuna matumaini. Lazima kuwe na chemchemi ya utajiri wa Mungu, ya Nguvu Zake za uponyaji, iliyofunguliwa mahali fulani, au hungetamani Hilo kamwe. Lazima iwe mahali fulani!

⁸⁵ Ikiwa unatamani kumwona Yesu huyo, ikiwa kitu fulani kinakufanya utamani kumwona Yehova, Yeye yuko mahali fulani au hutawahi kuwa na shauku hiyo. Mungu ni mwema kwako tu sawa na vile alivyo kwa wenye hekima au kwa yeyote. Ikiwa unamwonea Yeye kiu, “Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa maana wataletwa kwenye Chemchemi hiyo ambapo wanaweza kunywa sehemu ya kushibisha.”

⁸⁶ Huenda kuna watu wanakufa hapa. Hutaki kufa, unahisi kuna kitu ulichoachiwa. Hiyo ndiyo sababu uko hapa. Kunaweza kuwa na wenye fadhaa, ambapo huwezi hata kuweka mawazo yako pamoja; lakini kitu ndani yako kinakuambia, “Kuna Kitu ambacho kinaweza kunirudisha papo hapo tena.” Huenda kuna makahaba ambao wametembea mitaani, katika aibu; huenda kuna wanawake ambao wameishi bila haki kwa waume zao, na kuvunja nadhiri zao za ndoa; huenda kuna wanaume ambao ni walevi, wamefanya kila kitu kilichopo kwenye kalenda ya dhambi; lakini Kitu fulani kinakuambia kuna Chemchemi mahali fulani.

⁸⁷ Unaweza kuwa Mkatoliki, unaweza kuwa Myahudi, unaweza kuwa chochote ulicho, lakini wewe ni mwanadamu ambaye aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Naye anavuta kwako, akikuita, nawe unaongozwa kama vile wale wenye hekima walivyoongozwa.

⁸⁸ Na walipokuwa wakisoma, na kutazama kule na kuona hiyo Nuru, hawakuweza kujua ilikuwa ni nini. Na hebu tufikirie kuwa wao... Kesho yake walijilaza chini, ili wapate usingizi. Walitatizwa, na wakaendelea kuitazama. Ndipo mmoja wao hapana shaka aliota ndoto, Bildadi, tungesema aliota ndoto. Naye akaota ya kwamba kulikuwa na unabii uliosema, “Kutakuwa na Nyota ya Yakobo itakayotokea. Na mahali fulani huko, miongoni mwa Wayahudi, kuna mtoto Mfalme ambaye atazaliwa. Na hiyo Nuru unayoiona sasa itakuleta kwenye Nuru kamilifu ambayo itawaangazia kila mtu anayetafuta Nuru, inayokuja ulimwenguni.”

⁸⁹ Unaona, haidhuru kulikuwa na dini gani, kama kweli wanamcha Mungu, Mungu anawajibika kuwaleta kwenye Nuru hii. Anawaleta kwa njia yao wenyewe.

⁹⁰ Wakati mwingine Yeye huwaleta kwa mateso. Wakati mwingine Yeye huwaleta... Unajua, katika siku hizi za mwisho, Yeye alitabiri ya kwamba wangekuja kwa dhiki. Aliandaa chakula hiki cha jioni, na kisha hakuna—hakuna mtu aliyekuja, kisha akasema, “Enendeni katika njia kuu na vichochoro vya mji, mkawalete vilema, viwete, vipofu, na wanaoteseke, kwa maana meza Zangu zitajaa.”

⁹¹ Anawatafuta kutoka kila tabaka na kila kona ya maisha, kila mahali, wakitembea katika Roho katika siku hizi za mwisho, kuwaleta pamoja. Madhehebu yote, na wote ambao—ambao wanatamani uzima, wanayo haki ya kuupokea, kutembea katika Uwepo Wake, wa Utu Wake mtukufu, kwa maana Yeye ni Mwana wa Mungu aliye hai, Nyota ya Asubuhi ingali ikiangaza kati yetu, kama Yeye alivyoangaza daima.

⁹² Nuru iyo hiyo iliyomwangusha Paulo chini, akiwa njiani kwenda Dameski! Mnyofu moyoni mwake, akijaribu kutesa kundi la watu waliokuwa wakipiga kelele sana, wakipaza sauti, wakipiga kelele nyingi sana; alishuka kwenda kuwapiga, naye alifikiri alikuwa sahihi. Na hapo ilisimama ile Nguzo ya Moto katika njia yake, iliyomwangusha chini. Akapaza sauti, “Sauli, kwa nini unaniudhi?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu,” Yehova ambaye alikuwa na bidii juu yake.

⁹³ Alikuwa na bidii kwa Yehova. Hakujua lolote kuhusu Yesu, ila tu, “Alikuwa m—mhalifu.” Lakini Mungu alimtuma, naye akawa mmishenari mkuu zaidi ambaye ulimwengu umewahi

kumwona. Kwa nini? Alikuwa mwaminifu; aliamini. Mungu alimwongoza kwa Nuru.

⁹⁴ Je, unafikiri nini kinachotufanya tujisikie leo, kama Wakristo, kuona hata picha Yake? Nami ninayo moja sasa ambayo ni bora zaidi, mara mamia. Lakini Yehova Mungu yeye yule ametuma Nuru Yake, kabla ya Kuja kwa Mwanawe mara ya pili, kutuongoza, kutufariji, na kutuleta katika Chemchemi hiyo; ili tuoshwe kutokana na dhambi zetu, na tuwe safi katika haki ya Mwanawe, Bwana Yesu, na kufanyika wana na binti za Mungu, waliozaliwa upya na Roho wa Mungu, ambaye hubadilisha.

⁹⁵ Kuzaliwa kunamaanisha kuwa tumebadilishwa kutoka kwa mawazo yetu, tumebadilishwa kutoka kwa mitazamo yetu, tumebadilishwa na kitu fulani kilichotukia, ndani. Hakuna dini duniani, hakuna maji ya kutosha, hakuna namna za ibada au mahubiri ya kutosha, ambayo yanaweza kukubadilisha. Inahitaji Damu ya Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Hungeweza kujisafisha mwenyewe, kwa kujiunga na kanisa, kama vile chui asingeweza koundoa madoa yake kwa kuyalamba. Kadiri anavyozidi kulamba, ndivyo yanavyozidi kung'aa. Anayaonyesha tu. Kwa kujiunga na makanisa na kujaribu kufanya wema wako mwenyewe, unaonyesha tu ukosefu wako, wa njaa ndani, kitu ambacho hakijajazwa bado. Acha kujaribu; pokea tu. Yeye hukuongoza kwenye Nuru.

⁹⁶ Na kama watu hawa wenye ndoto hii, ya kwamba hawana budi kumwabudu Mtoto huyu, hawana budi kwenda. Na walikuwa matajiri. Wakakusanya mali zao na kuziweka katika hazina, kama ubani, dhahabu na manemane. Watatu walikwenda, kwa ajili ya ushahidi. Na wakatandika ngamia zao, wakatoka, wakiifuata ile Nyota. Hapana shaka walipanda juu ya mlima, wakashuka na kuvuka Mto Tigri kwenye kivuko, na kushuka hadi kwenye bonde la Shinari. Na ile Nyota ilikuwa ikiwaongoza mpaka Yerusalemu.

⁹⁷ Kwa maana, Yerusalemu daima imekuwa makao ya kidini ya ulimwengu, kwa maana Mfalme mkuu aliishi huko. Ilikuwa ni katika mji uo huo, ambapo palikuwa na Mfalme aliyekutana na Ibrahimu akitoka katika kuwaua wafalme, na Jina Lake lilikuwa Melkisedeki. "Hakuwa na baba wala mama; hakuwa na mwanzo wa siku, wala mwisho wa maisha." Hata mzee wetu, Ibrahimu, alilipa sehemu ya kumi, zaka, Kwake. "Hana baba, wala mama; hana wakati alipopata kuanza, wala wakati ambapo Yeye atakwisha." Ni Mfalme mkuu aliyetoka Salemu, ambayo ilikuwa Yerusalemu.

⁹⁸ Na ile Nyota ikawaongoza hawa mamajusi kwenye kiti cha kidini cha ulimwengu, lakini, jambo la kuhuzunisha lilikuwa, walipofika kule, hawakujua lolote kuihusu. Nao hawa mamajusi walienda huku-na-huku mitaani. Ile Nyota, mara tu walipofika Bethlehemu...Mara walipofika Yerusalemu, ilitoweka, kwa

hivyo haikuwaongoza tena. Mungu alikuwa anafanya nini? Akionyesha tu... jinsi ambavyo watu wanaweza kuwa.

⁹⁹ Hata hivyo, katika theolojia yetu yote na makanisa yetu makuu, na—na kadhalika, leo, wakati Nuru kuu ya Mungu imeanza kuangaza, kanisa halijui lolote kuihusu. Je, Vatikani inajua nini kuhusu mambo haya? Je, mashirika ya kanisa yanajua nini? Hakuna kitu! Tuko kwenye Krismasi nyingine.

¹⁰⁰ Watu hawa walijua ya kwamba walikuwa wameona kitu fulani. Walijua ya kwamba kulikuwa na jambo fulani lililokuwa limetukia. Kwa maana, walisoma sayari za juu, na hapa kulikuwa na Mgeni, nao walikuwa wameongozwa naye kiajabu. Na sasa, mjini, wanaenda huku-na-huku katika kila barabara ndogo, wakisema kwa sauti kuu, “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tumeiona Nyota Yake Mashariki.”

¹⁰¹ Sasa, wao walikuwa Mashariki, waliona Nyota Yake huko Magharibi. Lakini wakasema, “Tulipokuwa Mashariki,” mamia ya maili. Unaona, iliwachukua miaka miwili kumaliza safari.

¹⁰² Ninajua hilo linaangusha baadhi ya mafundisho yenu, lakini ni Kweli. Iliwachukua miaka miwili kumaliza safari. Hawakuja kama hawa wanaojiita Wakristo siku hizi, kuwa na mtoto wao mchanga katika hori amelala pale, na wale mamajusi wakija. Huo ni ujinga wa Kikristo. Kamwe hawakuja kwa mtoto mchanga kwenye hori. Hakuna Maandiko yanayosema walifanya. Walikuja kwa Mtoto mdogo, mwenye umri wa miaka miwili. Hakuwa horini. Alikuwa ndani ya nyumba. Soma Maandiko hayo mengine. Lakini mapokeo ya Kikristo, loo, wameuchanganya ulimwengu mzima na mafundisho yao.

¹⁰³ Kwa nini Herode akawaua watoto, wenye umri wa miaka miwili, basi, kama alikuwa mtoto mchanga tu? Maandiko yalisema walikuja kwa “Mtoto mdogo,” si mtoto mchanga; “Mtoto mdogo,” umri wa miaka miwili. Naye Herode akawaua watoto, hadi umri wa miaka miwili, kujaribu kumpata; ingekuwa watoto wachanga, hangelizimika kuchukua hadi miaka miwili, watoto wachanga tu.

¹⁰⁴ Hawakumpata kamwe horini; walimkuta ndani ya nyumba. “Na walipofika nyumbani, walimkuta Mtoto na Mariamu.” Lakini unaona jinsi wanavyoipindua.

¹⁰⁵ Si ajabu! Siku chache zilizopita usiku, nilikuwa nikihubiri kile Yesu alichowaambia wale Mafarisayo, “Mmeyashika mapokeo yenu, na kuzitangua amri za Mungu.”

¹⁰⁶ Kisha wanalia, “Mungu yuko wapi?” Unawezaje kumwamini Mungu wakati hutaamini Neno Lake, na kusema, “Yuko wapi huyo Mungu wa Biblia?” Rudi Kwake jinsi Yeye alivyo, hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kumjua Yeye. Hii *hapa* njia.

¹⁰⁷ Walienda huku na huko mitaani, wakilia, “Yuko wapi? Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliona Nyota Yake tulipokuwa Mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.”

¹⁰⁸ Loo, ninaweza kuona baadhi ya makuhani wakisema, “Aise, mabwana, hapana shaka mlisikiliza kundi la washupavu mahali fulani. Hapana shaka mnasikiliza theolojia duni ya mtu fulani.”

¹⁰⁹ Wanaume hao wangeweza kusema, “Hapana, bwana! Tuliiona ikifanya kazi. Tunajua ya kwamba ni halisi. Na imetuongoza kufikia umbali huu. Lakini hatuwezi kuipata tena, na huu ndio mji wa mfalme.”

¹¹⁰ Je, si ajabu hiyo? Kanisa kubwa kuliko yote ulimwenguni, watu wengi zaidi, hata hivyo hawakujua lolote kuihusu. Na kama hiyo si hali ile ile ya watu duniani kwenye Krismasi hii, hali ile ile! Hakuna aliyekuwa na jibu. Hawakuweza kupata jibu.

¹¹¹ Na hatimaye ikawa mbaya sana! Hawa walikuwa matajiri, unaweza kujua jinsi ngamia wao walivyokuwa wamepambwa. Wala hawakuacha mtaa mmoja; kila uchochoro, walienda wakipiga mayowe, “Yuko wapi? Yuko wapi? Yuko wapi?”

¹¹² Na leo huku mabomu ya atomiki yakining’inia kule kwenye maghala, leo wakati dunia iko kwenye ukingo wa maangamizi kamili, na kizazi hiki cha watu kuangamia kwa sekunde moja; kwa mvuto mmoja, taifa lolote dogo linaweza kuizamisha dunia.

¹¹³ Katika mkutano wa wanasayansi, hivi majuzi, walisema kulikuwa na utusitusi. Mbona, bomu la atomiki ni bastola ya kuchezea, kwa kile walicho nacho sasa. Na mataifa mengine yanacho. Ikiwa Pentagon ingeachilia walicho nacho, hakungekuwa na roho ya Krismasi iliyobaki, watu wangekuwa wakikimbia kwa hofu barabarani, wakipiga mayowe na kulia. Usingeweza kujificha. Hakuna njia ya kujificha.

¹¹⁴ Mwisho ni sasa. Tuko mwisho, ishara na maajabu yakitokea, Masihi akijidhihirisha Mwenyewe katika Roho.

¹¹⁵ Roho huyo, akishuka kote katika wakati, akijiumba Mwenyewe zaidi na zaidi, hata hatimaye akazaliwa ndani ya Mtu huyo mkamilifu.

¹¹⁶ Sasa katika nyakati za Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, na kushuka hadi mwisho, na sasa hapa inadhihirishwa kabla tu Yeye hajarudi katika mwili wa kawaida, Yule mkamilifu; akiliunganisha Kanisa Lake, akiwatoa katika kila dhehebu, kila kitu, akiwaleta Kwake, kwa maana Yeye atatokea hivi karibuni. Na makanisa hayana jibu.

¹¹⁷ Kwa hiyo Baraza la Sanhedrin liliitwa, na Herode mkuu wa mkoa, na mahakama zikakusanyika. Nao wakawaleta makuhani na marabi. Wakasema, “Soma Maandiko. Masihi huyu atazaliwa wapi?” akasema mfalme.

¹¹⁸ Na jambo la ajabu, unajua walimpata wapi? Katika unabii wa Mika. “Wewe, Bethlehemu ya Uyahudi, si wewe ndiye mdogo kuliko wakuu wote wa Yuda? Je, wewe si mtakatifu anayejibingirisha? Je, si wewe ndiye m—m—mdogo kuliko wote? Lakini kutoka kwako atatoka Mtawala wa watu Wangu.” Hapo ndipo walipoipata.

¹¹⁹ Na kwa hiyo wenye hekima, waliposikia hivyo, wakalipiga lango! Na mara walipoondoka mahali hapo pa kale, baridi, paliporudi nyuma, hapo ndipo ile Nyota ilining’inia tena. Nyota ilikuwepo. Na Biblia ilisema, “Walifurahi kwa furaha kubwa mno.” Loo, naweza kusema walipaza sauti kidogo, walipogundua, ya kwamba kile cha Kimbinguni chenye baraka ambacho walikuwa wamekiona, walipotoka katika njia hizo za kale, baridi, za kawaida, kilitokea tena. Hicho hapo.

¹²⁰ Nayo ikawaongoza mpaka Bethlehemu, ambapo walimwona Yule, ambapo Yeye, ambaye alikuwa Imanueli, alikuwa akilelewa katika duka la seremala, maskini. Nao wakatoa mizigo yote waliyokuwa nayo, wakaiweka miguuni Pake. Nao wakamwabudu kwa sababu walijua Nuru ilikuwa imekuja, na Mwokozi wa ulimwengu alikuwa anazaliwa. Walitoa, walitoa kila kitu walichokuwa nacho, kwa sababu Mungu alikuwa ametoa!

¹²¹ “Mungu aliupenda sana ulimwengu,” rafiki, huo ni mimi na wewe, “hata alimtoa Mwanawe pekee, kwamba yeyote,” Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, kafiri, chochote ulicho, “yeyote amwaminiye, asipotee bali awe na Uzima wa Milele,” unachotafuta. Kuwa na Uzima!

¹²² Na katika saa tunazoishi sasa, na kule kuja kwa Utu Wake tena duniani, kulikokaribia, kama ukiona Maandiko.

¹²³ Angalia Yusufu alikuwa nani, tazama Roho wa Kristo ndani ya Yusufu. Alichukiwa na ndugu zake kwa sababu alikuwa wa kiroho, aliona maono, lakini alipendwa na baba yake. Huyo si alikuwa Yesu? Aliuzwa kwa yapata vipande thelathini vya fedha, na ndugu zake, kama Yesu alivyouzwa. Akasalitiwa, kama Yesu alivyosalitiwa. Akatupwa kwenye shimo, awe amekufa, kama Yesu alivyokuwa. Akainuliwa na akawa mkono wa kuume wa Farao, hakuna mtu angaliweza kuja kwa Farao isipokuwa kupitia kwa Yusufu. Na Yusufu alipokuja kutoka—kutoka mkono wa kuume wa Farao, walipiga kelele, “Piga goti, kwa maana Yusufu anakuja!”

¹²⁴ Biblia ilisema, kwamba, “Atakapokuja, kama radi inavyotokea Mashariki hadi Magharibi, kwamba kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu.” Mataifa yote yataomboleza na kutetemeka wakati huo.

¹²⁵ Ilikuwa ni nini? Ilijidhihirisha karibu zaidi, ikamjia Daudi, mfalme. Maana, Yeye alikuwa ni Nabii, Kuhani, na Mfalme pia; na wakati Daudi alipoondolewa mamlakani na kukataliwa,

huko Yerusalemu, kama Yesu alivyokuwa, Daudi aliketi juu ya mlima, mfalme aliyekataliwa, na watu wake mwenyewe, na akaulilia Yerusalemu. Naye Mwana wa Daudi akaja na kuketi juu ya mlima ule ule, Mfalme aliyekataliwa katika mji Wake Mwenyewe, akalilia Yerusalemu, akisema, “Ni mara ngapi ningekufunika kama kuku afunikavyo vifaranga vyake, lakini hukukubali.”

126 Walimwitaje? “Beelzebuli, mpiga ramli, pepo mchafu.”

127 Wakati huduma Yake ilipoanza, kulikuwa na mzee mvuvi aliyeletwa Kwake, ambaye hakuweza hata kuandika jina lake mwenyewe. Ndipo akamtazama huyo mzee mvuvi, Naye akamwambia jina lake lilikuwa nani. Naye akamwambia jina la baba yake lilikuwa nani. Huyo mzee mvuvi alimwamini, kwa moyo wake wote.

128 Na mwingine aliyesimama pale, akaongoka, jina lake Filipino. Naye akazunguka mlima, maili thelathini, akamkuta mmoja jina lake Nathanaeli, chini ya mti, akiomba. Akasema, “Njoo, uone Yule tuliye mpata. Ninajua wewe ni mwaminio hodari katika Yehova. Najua ndivyo ulivyo. Lakini Yehova anaahidi Masihi, nasi tumempata. Yeye ni Mtu wa kawaida tu, hakuna jambo kubwa Kwake. Hakuna kitu kikubwa na chenye elimu juu Yake. Yeye ni Seremala.” Alikuwa—Yeye alikuwa Seremala, wa nyenzo na roho ya mwanadamu pia.

129 Ndipo Nathanaeli akamtazama, akasema, “Sasa ngoja kidogo, je, laweza lolote jema kutoka Nazareti?” Unaona, walikuwa wakiitarajia kutoka Yerusalemu.

130 Hapo ndipo wengi wenu mnapotazama leo. Usiangalie hapo. Ibilisi daima hutumia kichwa cha mtu na macho yake. Mungu anatumia moyo wake. Unaangalia na kusema, “Loo, haiwezekani kabisa. Haina mantiki. Unaona, naweza kusema, naweza kuiangalia.” Hapo ndipo ibilisi akaapo. Ibilisi hutumia macho ya mtu. Alimfanyia Hawa hivyo, hapo mwanzo, na amefanya hivyo tangu wakati huo.

131 Lakini, Mungu humwambia mtu anaishi, moyoni mwake, na moyo wako unakufanya uamini mambo ambayo huwezi kuyaona. Kwa sababu, “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni ushahidi usiouona.”

132 Hakika, kanisa hili kuu pamoja na watu wake wakuu wote, mamilioni yake yote kote ulimwenguni, linadhibiti nguvu za ulimwengu, linapaswa kuwa kubwa. Usiangalie hilo.

Ni Roho, Roho!

Nathanaeli alisema, “Je, kitu chochote kizuri kinaweza kuja?”

Akasema, “Njoo, uone.”

133 Naye alipomwona akija, Yesu alimwangalia, na Yeye alikuwa anaenda kufanya ishara Yake ya Kimasihi juu yake. Akasema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

134 Akasema, “Ulinijua lini, Rabi?” Hilo lilimshangaza. “Ulinijua lini?”

135 Kasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.” Angewezaje kumwona, maili thelathini kuzunguka mlima, siku iliyotangulia?

136 Ambaye mwujiza ulifanywa juu yake, akatazama juu na kusema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.”

137 Yesu akasema, “Kwa sababu nimefanya hivi mbele zako, nawe ukaamini, utaona makubwa kuliko haya, kwa maana kutakuwa na wakati unaokuja ambapo utaona Malaika wa Mbinguni wakishuka.”

138 Hapo karibu walisimama wale, hata hivyo, ambao walikuwa werevu. Walikuwa wa kanisa kubwa, wao—wao hawakuweza kujiondoa wenyewe. Wakasema, “Mtu huyu ni mpiga ramli. Yeye ni Beelzebuli. Ana kichaa. Yeye ni Msamaria ambaye ana pepo mchafu juu Yake. Ana wazimu.” Wakamtangaza hadharani, kuwa ni mwendawazimu.

139 Na Yesu akasema, “Kwa sababu umeniambia hivyo, nitakusamehe kwa hilo. Lakini kutakuja wakati ambapo Roho Mtakatifu atakuwa duniani, na atafanya kile kile ninachofanya.” “Neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Wazia hilo! Neno moja dhidi Yake, ndilo lote, linakutia muhuri milele.

140 Tunaishi wapi? Tuko kwenye Krismasi tena. Sijui kama dini yetu imetuleta karibu vya kutosha na Mungu, hata tuweze kuongozwa kiasi ambacho Mamajusi waliweza kuongozwa?

141 Sasa, kumbukeni, kuna watu watatu tu duniani, hata hivyo: watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; huyo ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

142 Sasa, Wayahudi na Msamaria wote walikuwa wakimtazamia Yeye kuja; sio sisi watu wa Mataifa. Tulikuwa makafiri, tumechukuliwa na sanamu bubu, katika siku hizo; fimbo mgongoni mwetu, rungu, kuua, kula kile tulichoweza; Mataifa, mbwa bubu.

143 Lakini walikuwa wakimtazamia Masihi, nao wakakosa kuona kwa sababu hawakutambua ishara Yake. Hiyo ndiyo sababu Yerusalemu haikuwa na jibu.

144 Hiyo ndiyo sababu, leo, hawana jibu. Mungu analo jibu, peke yake.

¹⁴⁵ Waangalie hawa kwa muda mfupi tu, kama walivyokuwa. Kulikuwa na tabaka lingine la watu wakimtafuta, hilo ni katika Yohana Mtakatifu 4, hao ni Wasamaria. Waliamini kulikuwa na Masihi ajaye.

¹⁴⁶ Kwa hiyo kumbukeni, Yeye hakuwahi kufanya ishara hiyo wakati mmoja mbele ya Mataifa, Wasamaria tu na kwa—na kwa Wayahudi, waliokuwa wanamtazamia Yeye kuja. Nao hawakumwamini, kwa hilo; baadhi yao walimwamini, wengine hawakumwamini.

¹⁴⁷ Naye alipokuja Samaria, aliwatuma watu, wanafunzi Wake, waende mjini. Akasubiri. Kwa sababu, aliwaambia, “Nendeni mkanunue chakula.” Ilikuwa karibu wakati huu wa mchana, nadhani.

¹⁴⁸ Walipokuwa wameenda, mwa—mwanamke mzuri akaja kisimani, kuchota maji. Loo, tunamwita kahaba. Labda alikuwa. Vema, hebu tuseme alikuwa mwa—mwanamke mwenye sura nzuri. Alitoka akaja kwenye kisima hiki, kuchota maji. Naye akasikia sauti, ikisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹⁴⁹ Naye akatazama huku na huku, na hapo Myahudi ameketi. Sasa, kulikuwa na ubaguzi wakati huo, hawakuwa na uhusiano wowote. Naye akamwambia, akasema, “Kwa nini, Wewe, Myahudi, unaniuliza mimi mwanamke Msamaria? Hatuna mahusiano sisi kwa sisi. Si sawa kwako Wewe kuniuliza hivyo.”

¹⁵⁰ Akasema, “Lakini, mwanamke, kama ungejua ni Nani uliyekuwa ukizungumza naye, ungeniomba Mimi Maji.”

¹⁵¹ Akasema, “Iko wapi...Unaweza kupata wapi maji,” kasema, “Huna chochote cha kuchotea, na kadhalika.”

¹⁵² Naye akaendelea na mazungumzo, wakati mwendo ukiendelea. Hatimaye, akamwambia, alipata mahali shida yake ilipokuwa. Akasema, “Mwanamke, nenda kamwite mumeo mje hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

¹⁵³ Akasema, “Hiyo ni kweli. Umeolewa mara tano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako.”

¹⁵⁴ Angalia alichosema. Walikuwa wakimtazamia Masihi, mwajua. Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.” Haya basi. “Naona kuwa Wewe ni nabii. Tunajua, Masihi atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya. Ishara ya Masihi, tunajua kwamba Masihi atafanya hivi wakati atakapokuja. Lakini Wewe tu ni...una michubuko mkononi mwako. Wewe ni Seremala, na Myahudi. Lakini hapana shaka Wewe ni nabii, la sivyo hungeweza kufanya hili. Lakini Masihi atakapokuja... Tunamtazamia hapa. Atakapokuja, atafanya hivi.”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema na wewe, Ndiye.” Loo, jamani!

¹⁵⁵ Akaangusha ule mtungi wa maji. Akaingia mjini, akasema, “Njoooni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Na mji wote ukatoka na kumwamini, naam, kwa sababu ishara hiyo ilifanywa. Mekanisa hayakuwa na jibu, lakini wanyenyekevu moyoni humtazamia Mungu.

¹⁵⁶ Leo, najiuliza kama dini yetu imetufikisha kwenye hiyo Akili? Kutambua kuwa si katika theolojia yetu yenye manukato iliyotengenezwa na mwanadamu ambayo tunajaribu kufundisha, bali ni katika Nguvu na ufufuo wa Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu nchini leo. Ndugu, dada, katika saa hii ya mwisho, inapokaribia mwisho wa wakati, zichunguzeni nafsi zenu, mjue jinsi mnavyosimama na Mungu.

¹⁵⁷ Ni Krismasi. Mapambo yote, pilkapilka zote barabarani, za Baba Krismasi, hadithi ya kubuni ya Kijerumani, fundisho la sharti la Kikatoliki, hakuna hata sehemu moja yake iliyo kweli. Na inachukua mahali pa Yesu Kristo, katika mioyo ya Wamarekani wengi sana. Krismasi haimaanishi Baba Krismasi. Krismasi maana yake Kristo. Si mtu fulani aliye na kiko kinywani mwake, na akishuka kwenye dohani! Ukiwafundisha watoto wako vitu kama hivyo, unatarajia wakue wawe nini? Waambie Ukweli, sio kwenye hadithi fulani za uwongo. Waambie, “Kuna Mungu wa Mbinguni ambaye alimtuma Mwanawe, na hiyo ndiyo maana ya Krismasi. Naye yuko karibu kuja tena.”

¹⁵⁸ Na shinikizo linapoanza kuja duniani, ibilisi ametoa vitu vyake, kwa macho, vile unavyoweza kuona, mapambo, na kadhalika. Mungu ametoa Yake, ambayo ni Roho, ambayo huwezi kuona, lakini unaamini.

¹⁵⁹ Yerusalemu haikuwa na jibu. Jeffersonville haina majibu; Louisville haina, Marekani haina, wala ulimwengu hauna.

¹⁶⁰ Mungu anayo majibu, na Yeye ameahidi ya kwamba atayadhihirisha. Nami ninakutangazia ya kwamba Yesu yeye yule, aliyezaliwa miaka elfu moja na mia tisa, anaishi leo, kutokana na ufufuo, na ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁶¹ Je, unaamini hili kwa dhati kwa moyo wako wote? Ikiwa unaamini. . . Na labda hujawahi kuikubali hapo awali, lakini, kabla ya Yeye kufanya jambo moja ili kujidhihirisha Mwenyewe, mwaweza kuinua mikono yenu? Kwa kuinua mikono yenu, huku kila mtu akiwa ameinamisha vichwa vyao, mngeinua mikono yenu na kusema, “Ndugu Branham, niombe. Ninaamini ya kwamba hiyo ni Kweli. Nami naamini ya kwamba kwa namna fulani, kwa njia ya ajabu, nimeongozwa kwenye maskini mahali hapa pa zamani kwenye kona asubuhi ya leo. Nami naamini ya kwamba Roho wa Mungu aliye hai yuko hapa sasa. Ninataka

kumwabudu. Nitainua mkono wangu.” Mungu akubariki. Hiyo ni nzuri. Loo, jamani! Watu ishirini au thelathini, kote jengoni.

¹⁶² Mungu Mpendwa, Wewe unaiona mikono hiyo, na Wewe unajua kila mmoja wao. Nao wana uhitaji. Nao wasingeinua mkono huo kamwe isipokuwa Kitu fulani kilikuwa karibu nao, Ambaye alikuwa mkuu kuliko wao; wangeendelea kwa njia zao wenyewe. Bali wameamini, kwa kusikia Neno. Maandiko yetu yanatambia, Bwana, Maandiko Yako Matakafu, kwamba, “Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu.” Na ni njia mbovu, rahisi, hata hivyo, njia—njia pekee tuliyo nayo kuiwasilisha kwa watu, wao wameiamini. Mikono mingi, mingi imeinuliwa. Sijui hata mmoja wao. Wewe unawajua wote. Lakini najua kwamba ndani yao, wanatawaliwa na kuongozwa na roho, na hiyo roho iliyo ndani yao imesema, “Umekosea.”

¹⁶³ Na kuna Roho mwingine aliyesimama karibu nao, akisema, “Nikubali Mimi. Mimi ni Mwokozi wako.” Nao walivunja kanuni zote za kisayansi, kwa kuinua mikono yao. Kwa sababu, kuna Mungu mle ndani, Ambaye alitunga kanuni za kisayansi, na mikono yao ikainuliwa, kwamba walitaka kufika juu, kwa imani, kumshika Mwokozi, na kumkubali kama Mwokozi wao. Wamefanya hivyo asubuhi ya leo, Bwana.

¹⁶⁴ Na uwapokee katika Ufalme Wako, sasa hivi. Wao ni nyara za Ujumbe. Ninaomba ya kwamba utawapokea katika Uwepo Wako, katika Ufalme Wako. Na waishi maisha ya furaha hapa, wakitazamia Kuja kwa Bwana Yesu wakati wowote, wanapoona siku ikikaribia, na ishara na maajabu, kwa maana Yeye anakaribia, anakaribia zaidi. Yuko njiani.

¹⁶⁵ Kama Rebeka alivyoinuka, ameketi kutagaa juu ya ngamia, akaenda kumlaki Isaka, mpenzi wake. Na Isaka alikuwa tayari ameondoka ka—kambini, naye alikuwa nje kondeni, wakati wa jioni, alipomwona akiya. Ilikuwa ni upendo kwa kuonana mara ya kwanza. Aliruka kutoka kwa ngamia, na kukimbia kumlaki. Alipelekwa katika hema ya Ibrahimu, na hapo akawa mrithi, na kurithi vitu vyote.

¹⁶⁶ Mungu, tunatambua kuwa ni wakati wa jioni sasa. Ulisema itakuwa Nuru, kwamba Roho Mtakatifu atakuwa hapa duniani na atakuwa akijidhihirisha Mwenyewe katika kundi dogo ulilolichagua kwa neema Yako. Ninaomba sasa ya kwamba Wewe—Wewe utajidhihirisha Mwenyewe kwa njia kuu kwa kila mmoja. Na hebu waokolewe na dhambi zao.

¹⁶⁷ Pia jalia waje mahali fulani kwenye che—chemchemi, chemchemi ya duniani, baada ya wao kufika kwenye cha Kimbinguni, na wabatizwe katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu; wakioshwa dhambi zao, wakiliitia Jina la Bwana. Jalia wampokee Roho Mtakatifu, na kuwekwa katika nafasi ili kutimiza sehemu yao ya mchezo huu mkuu wa kuigiza unaokaribia kufanyika.

168 Tunaamini kukusanyika kwetu asubuhi ya leo, Baba, kulikuwa katika jimbo Lako lenye hekima. Hakuna kitu kijinga, Kwako. Kila kitu, kila kitu unachotoa Wewe, ni kikamilifu. Wanaume na wanawake wamekuja kutoka sehemu mbalimbali za nchi, wameketi hapa ndani. Uliwaleta kwa Roho Wako, kwa njia ya ajabu. Wamekuamini Wewe. Wapokee sasa. Katika Jina la Yesu Kristo, ninawawasilisha Kwako.

169 Sasa, Bwana, jalia Roho Wako Mtakatifu aje kuponya wagonjwa, ili hawa waongofu wapya Kwako, waweze kutambua ya kwamba hatuzungumzii tu Biblia ambayo imekuwa historia. Ni wakati ulio hai, uliopo, sasa hivi. Yeye ni Bwana Yesu yule yule.

170 Sasa jalia aje, Bwana, na atwae miili yetu, miili yetu, tunapofungua mioyo yetu. Ondoa mashaka yote na ulimwengu wote. Na umruhusu tu Roho Mtakatifu atembe ndani yetu, ili uweze kufanya mapenzi Yako kati yetu, kama vyombo safi. Si kwa sababu sisi tu safi kwa haki yetu wenyewe, bali kwa sababu tumemwamini Yeye aliyetusafisha, Bwana Yesu; na ametenda na kufanya ma—mambo uliyofanya Wewe ulipokuwa hapa duniani, ili waongofu hawa wapya wapate kuona kwamba Wewe ungali Bwana Yesu. Hujafa. Lakini ulifufuka tena, miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, na uko hai leo, ukitimiza kila ahadi uliyotoa. Amina.

171 Najua si wimbo wa Krismasi, lakini ni wimbo wa mioyo yetu, ambao tunaupenda; sasa kwa kuwa ujumbe umekwisha, kwa namna fulani unakata, na kadhalika, ndiyo njia pekee.

172 Kile ambacho mimbara yetu inahitaji leo si hii hapa dini yenye manukato. Inahitaji Ukweli. Kweli, ihubiri kutoka katika Biblia! Usifanye tafsiri zozote tofauti. Iseme tu, yale Biblia isemayo. Mungu anawajibika kwa Neno Lake. Asipolitetea Neno Lake, basi Yeye si Mungu, ama Hilo si Neno Lake, mojawapo. Bali atalitunza Neno Lake.

173 Sasa, kabla tu hatujawaombea wagonjwa, hebu na tumbe wimbo huu mzuri wa zamani, enyi watu wote, pamoja, ninyi nyote.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwani Damu Yake imeosha kila waa.

174 Unaweza kutupa sauti, dada? Kila mtu, pamoja sasa, wote, kila mtu!

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi,
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwani Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁷⁵ Nashangaa. Huku si kukufuru. Huku ni kujieleza tu. Watoto, sisi ni watoto. Unapofikia kufikiria kuwa wewe ni mtu mzima, katika Mungu, hiyo inaonyesha kuwa hujafika popote. Daima kuwa mtoto, Yeye anaweza kukuongoza. Lakini unapojua mengi kuliko Yeye, unajaribu kumwongoza. Unaona? Mwache akuongoze. Hebu na tufunge tu macho yetu na kuinua mikono yetu, na kuinamisha vichwa vyetu, na kuimba huo mara nyingine tena.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwani Damu Yake imeosha kila waa.

Kutoka hori ya Bethlehemu akaja mgeni,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani
hadi utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

Ili tu kuwa kama Yesu, kuwa tu kama Yesu,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani
hadi utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

¹⁷⁶ “Mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya.”

¹⁷⁷ Si ungetamani uwe umesimama pale wakati alipomwambia yule mwanamke aliyekuwa anatokwa damu? Alikuwa akijipinda katikati ya umati, akagusa vazi Lake, “Maana alisema moyoni mwake, ‘Huyo ni Mwana wa Mungu. Nikiweza tu kugusa vazi Lake!’” Sasa, vazi la Kipalestina lilipwaya, na lilikuwa na vazi la ndani. Yeye . . . Yeye kamwe hakuhisi mguso huo, kwa maana Yeye alithibitisha jambo hilo. Aligusa vazi Lake, naye akarudi haraka kwenye kusanyiko.

¹⁷⁸ Yesu akasimama, akasema, “Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?”

¹⁷⁹ Petro akamkemea, akasema, “Bwana, kila mtu anakugusa, wanakusalimia kwa mkono, wanakupigapiga, na kila kitu. Kila mtu alikugusa Wewe, basi kwa nini unasema jambo kama hilo Wewe?”

¹⁸⁰ Akasema, “Lakini nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka. Mtu fulani amenigusa.”

¹⁸¹ Naye akatazama huku na huku, juu ya kusanyiko, na akampata. Naye akamwambia ya kwamba alikuwa anatokwa na damu wakati huo, na imani yake ilikuwa imemponya.

¹⁸² Hvi usingependa kuwa hivyo? Sikuweza kufikiria chochote kikuu zaidi.

183 Mtu mmoja alimwendea. Akasema, “Jina lako ni Simoni. Jina la baba yako ni Yona.” Loo!

Ninaomba tu kuwa kama . . .

184 Inawezekana? Akasema, “Mambo haya ninayofanya! Na bado kitambo kidogo, na ulimwengu. . .” Sasa, *ulimwengu* pale, katika neno la Kiyunani, ni *kosmos*, ambalo linamaanisha “utaratibu wa ulimwengu,” sio ardhi, “utaratibu wa ulimwengu.” “Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona,” huyo ni mwaminio, “kwa maana Mimi,” na *mimi* ni kiwakilishi cha kibinafsi, “Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi ukamilifu wa dahari. kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Nyingi kuliko hizi mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Ahadi takatifu zilizobarikiwa, haziwezi kuvunjwa. Yesu alisema, “Hakuna Maandiko yanayoweza kuvunjwa.”

Kwa hiyo kuwa kama Yesu . . .

Je, Yupo hapa?

. . . Yesu,

Katika mtazamo wa kuabudu tu sasa.

Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani
hadi Utukufuni
Ninaomba tu kuwa kama . . .

185 Je, unaweza kuwazia Yeye akitembea Galilaya? Kuna wale Mafarisayo, waliosema moyoni mwao, “Yeye ni Beelzebuli.” Hawakusema hivyo kwa sauti, lakini alitambua mawazo yao. Maandiko yanasema hivyo? Alitambua mawazo yao.

186 Alisema, “Ukisema hivyo dhidi Yangu, nitakusamehe. Lakini utakuja wakati ambapo Roho Mtakatifu atafanya mambo yaya haya. Usinene dhidi ya Huyu.”

187 Ili tu kuwa kama Yesu! Ni wangapi katika kusanyiko hili dogo asubuhi ya leo wanaoamini ya kwamba amefufuka katika wafu, Yu hai leo, na Yeye ni yule yule, kutimiza kila ahadi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Asante. Hiyo inaleta Uwepo Wake.

188 Wengi wenu mnaijua picha ya Malaika wa Bwana, pale juu ya ninaposimama. Tunazo kutoka Ujerumani, Uswisi, kila mahali wanapozipiga. Walipiga moja hivi majuzi. Ndicho kitu cha kipekee zaidi ambacho nimewahi kuona. Nitaipeleka kanisani, wakati mwingine nitakaporudi. Iko katika o—ofisi za kitaifa sasa, kuchunguza kwa mfichuo maradufu, na jinsi ya kuwekwa chini ya mwanga wa mionzi ya jua, na kadhalika, kuona. Malaika wa . . . faraja kuu niliyopata tangu Yeye alipokutana nami; tunajua kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho.

189 Mimi ni mwanadamu, na hakuna kitu kizuri katika mwanadamu. Lakini kama mtu anaweza kuufungua moyo wake na kumwacha Mungu amsafishe, basi si. . . Mikono pekee aliyo nayo Mungu, hiyo ni mikono yako na mikono yangu; macho Yake ni macho yangu na macho yako, kwa maana Yeye ni Roho. Lakini anaweza kufanya kazi kupitia sisi, kudhihirisha na kufanya mapenzi Yake.

190 Nilitaka kuwaita hapa kwenye mstari wa maombi. Nimebadilisha mawazo yangu. Ninaamini ya kwamba Uwepo wa Bwana Mungu uko hapa. Nami ninaamini ya kwamba Yeye anaweza kufanya vile vile alivyofanya alipokuwa hapa hapo awali, la sivyo Yeye si Mungu. Ni watu wangapi. . .

191 Kuna nyuso nyingi hapa sijui. Sipo hapa; hata wengi wenu wanaweza kuja kanisani hapa, siwajui. Lakini ni wangapi humu ndani, ambao ni wahitaji, na unajua kwamba sikujui, inueni mikono yenu; wote walioko ndani ya jengo, mnajua. Hasa ni hapa mbele, karibu kila mtu hapa mbele, wageni kabisa.

192 Basi kama Yesu yu hai, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na ikiwa unalo hi—hitaji la kitu chochote, Maandiko yanasema. . . Sasa, si Agano la Kale; Agano Jipya! Agano Jipya, Kitabu cha Waebrania, kilisema, “Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu sasa hivi.” Kuna mtu anayejua kuhani mkuu ni nini? “Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Kuhani mkuu anatakiwa kufanya maombezi katika Uwepo wa Mungu. Yesu anasimama kama Kuhani Mkuu, kufanya maombezi, Naye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Sasa, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele; na kama mwanamke alimgusa kule nyuma, Naye akageuka na kumwambia; na kipofu Bartimayo amesimama langoni, yadi mia tatu kutoka pale alipokuwa, akipiga mayowe, “Nihurumie!”

193 Na watu wakimdhahi alipokuwa akipita, Yeye akiwa ameelekeza kichwa Chake Kalvari, akipanda kwenda Yerusalemu, kutolewa dhabihu. Na hao makuhani wakisema, “Aise, Wewe uliyefufua wafu! Tuna makaburi yaliyojaa hao hapa, njoo uwafufue. Tutakuamini.” Kundi lile lile lililosema, “Toka msalabani, (Wewe ni ‘Mwana wa Mungu’), nasi tutakuamini.”

194 Unawaona wakosoaji? Wamekuwa nao kila wakati. Usijiunge, usipige kura yako na wa aina hiyo. Mungu aepushe! Mweke Mungu moyoni mwako ili uweze kumwona na kumjua.

195 Lakini maskini huyu, mzee ombaomba kipofu aliyesimama pale, akasema, “Ee Mwana wa Daudi, nihurumie.” Na imani yake ikamsimamisha Yesu. Yesu aligeuka na kuangalia mpaka akamkuta, akamwambia atafunguliwa macho yake.

196 Yesu yuyo huyo yu hai! Kama. . . Mungu wa historia ana faida gani, Yeye hana. . . kama Yeye si Mungu yule yule leo?

¹⁹⁷ Inaleta faida gani, kujaribu kumpasha mtu joto kwa kumwelekeza kwenye moto uliochorwa? Moto uliochorwa hautafanya... Huo ni moto wa kihistoria. Unasema, “Si moto uliochorwa, Ndugu Branham, ni picha ya moto ambao kwa hakika ulitokea.” Huwezi kupata joto kwa picha. Hicho ni kitu ambacho kilikuwa. Na sasa je?

¹⁹⁸ Ni yeye yule jana, ama Yeye... na leo, ama Yeye si Mungu yeye yule. Je, hamwamini jambo hilo?

¹⁹⁹ Sasa kila mmoja wenu awe na kicho kabisa. Iwapo ningezungumza, sina njia ya kukujua. Mungu anaujua moyo wangu. Lakini ikiwa Yesu atakuja na kuchukua mwili wangu, na kuchukua mamlaka... Haijalishi ni kiasi gani angechukua mamlaka juu yangu, asipochukua mamlaka juu yako, pia. Huna budi kuliadini. Kwa maana, kumbuka, ni vile tu unavyoamini. Ikiwa Bwana Yesu atakuja na kufanya hivyo, na wewe utagusa vazi Lake, ukisema, “Bwana, mimi ni mhitaji. Jalia nikuguse Wewe, Bwana.”

²⁰⁰ Basi ukimgusa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, atatenda vile vile alivyofanya alipokuwa hapa duniani. Je, hiyo ni kweli? Kama likitenda kwa njia nyingine yoyote, basi ni jambo baya, umegusa jambo baya. Haina budi kuwa vile vile, inapaswa kutenda kwa njia ile ile. Basi kama unaweza kugusa vazi Lake, kama vile mwanamke alivyofanya aliyegusa vazi Lake, si Yeye angefanya jambo lile lile?

²⁰¹ Ikitokea kuwa mimi... Ikiwa baadhi yenu watu mnaokuja kwenye kanisa hili, ili ujue, si—sitakuambia chochote. Inabidi iwe ni imani yako, kwa sababu hii ni—hii ni... Mimi... Nataka wageni. Nitakupata baada ya muda mfupi, Bwana akipenda. Nataka... Nitakuleta hapa jukwaani, nikuombee.

²⁰² Nataka wageni ambao wametoka nje ya mji. Kama ninyi watu wa nje ya mji, mko hapa katika hoteli na moteli, na kadhalika, mnangojea. Hakika, kuja kutoka duniani kote, kwa njia hiyo. Wanampenda Bwana. Wanamwamini. Na wao—wanasoma katika Biblia kwamba Yeye anapaswa kufanya hivi katika siku za mwisho.

²⁰³ “Wala hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu,” alisema Yesu. Huwezi kuja, hakuna haja ya kujaribu kufanya lolote isipokuwa Mungu akuvute. Mungu anapokuvuta, basi utakuja. “Naye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe.”

²⁰⁴ Sasa wewe uwe na imani tu na uamini sasa. Na uwe na kicho kabisa, na utulie kwa muda kidogo. Mpe Mungu mawazo yako. Omba, ukisema, “Bwana Mungu, nijalie niguse vazi Lako. Mimi ni mgonjwa. Mimi ni mhitaji. Nina haja. Ndugu Branham hanijui, hii ndiyo mara yangu ya kwanza kumwona mtu huyo. Lakini ninataka kujithibitishia mwenyewe kwamba Wewe ungali Yehova, ya kwamba Wewe ungali ni Yesu

ambaye anazungumza habari zake. Nami ninaamini Nuru hii ya ajabu ambayo ulimwengu unazungumza juu yake siku hizi. Ninaamini ni Wewe. Na Wewe ndiwe yule yule uliyeniongoza hapa. Sasa nitapata nini? Hebu nimpate, Bwana, Yesu yeye yule waliyempata. Jalia nimpate.” Sasa tazama tu na uangalie.

205 Sina njia hata kidogo ya kujua hadi Mungu atakapoifunua. Na wakati Mungu anapoifunua, basi ni Mungu anayeifanya wakati huo, si mimi. Ni wangapi wataamini kama atafanya hivyo? Ninamngoja Yeye. Inueni mikono yenu. Unasema, “Nitaamini. Naam, bwana. Nitaamini, kwa moyo wangu wote.” Vema.

206 Sasa inueni vichwa vyenu, mnapotazama na kuomba. Sasa kwa upole sana, wimbo huu. Hii hapa piano ya zamani niliyousikia kwa mara ya kwanza.

Amini tu . . .

207 Yesu alishuka kutoka mlimani, wanafunzi Wake walikuwa wakijaribu kuponya ugonjwa wa kifafa. Hawakuweza kufanya hivyo, ingawa walikuwa na nguvu. Wakamletea Yesu. Akasema, “Naweza kama unaamini, kwa maana yote yanawezekana. Amini tu.”

208 Kila mtu mchaji uwezavyo kuwa. Angalia tu huku, kama Petro na Yohana walivyosema, “Tuangalie sisi.” Sio kuwaangalia kwa ajili ya kitu, lakini kuweka makini. Kasema, “Fedha na dhahabu sina.”

209 Mungu wa Mbinguni alijalie. Unaona, Neno Lake liko hatarini, si langu. Ninawajibika tu kulihubiri.

210 Ni ngumu, huu ni mji wangu wa nyumbani. Unajua, Yesu aliambiwa, alipoenda kwenye mji wa nyumbani Kwake Mwenyewe, hangeweza kufanya miujiza mingi. Ninyi nyote mnajua hilo. Ndipo Yesu akasimama basi, akasema, “Nabii hatakosa thawabu, isipokuwa ni katika mji wake mwenyewe, miongoni mwa watu Wake.” Hiyo bado ni nzuri leo.

211 Lakini kuna wengi hapa ambao sio wa mji wa nyumbani.

212 Mwishoni kabisa mwa safu pale, bwana, akinitazama, akiwa na miwani, nadhani hatufahamiani. Mungu anatujua sote wawili. Lakini unajua kuwa kuna kitu cha kushangaza kinaendelea. Kama ungeweza kuona kile ninachokiona, moja kwa moja juu yako kuna hiyo Nuru. Ikiwa Mungu atanifunulia! Sasa unawasiliana Naye. Itabidi atumie sauti yangu na macho yangu. Lakini unahitaji kitu. Sikujui wewe. Unajua sijui chochote kukuhusu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, bwana.

213 Lakini unatambua una kitu kama hisia, tamu sana, hisia ya unyenyekevu (Hiyo si ni kweli?) sasa hivi. Huyu ni Malaika wa Bwana. Yuko moja kwa moja juu yako. Ikiwa Mungu atanifunulia shida yako ni nini, kama tu alivyofanya kupitia

Mwanawe, Bwana Yesu; Naye alikuja kutakasa moyo wangu, ili apate kuishi hapa ili kusema nawe; je, utaamini kuwa ni Kuhani Mkuu yule yule ambaye umemgusa? Unawasiliana na Kitu fulani. Huyu ni Yeye.

²¹⁴ Shida yako iko kwenye mapafu yako. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Ni mbaya sana huwezi kufanya kazi. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Sikujui.

²¹⁵ Ni wangapi wanaoamini sasa? Angalia hapa. Unafikiri nilibahatisha hiyo. Roho bado yuko juu ya mtu huyo.

²¹⁶ Unaamini Mungu wa Mbinguni anakujua? Unamtumikia? Ninasema unamtumikia? [“Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ndiyo, bwana. Wewe ni Mkristo. Umekuja hapa kwa kusudi la kuponywa. Unaenda nyumbani, mzima. Jina lako ni Bw. Raney. Hiyo ni kweli kabisa. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Unaweza kurudi nyumbani. Umeponywa, bwana. Imani yako imekuponya. Mungu akubariki.

²¹⁷ Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu, hii hapa mikono yangu, labda mara yetu ya kwanza. Ni Mungu. Sasa kaa kimya. Kila mtu awe katika maombi. Unajua ya kwamba kuna Kitu hapa kinachofanya hivyo.

²¹⁸ Sasa, Mafarisayo walisema, “Yeye ni ibilisi.” Kisha wakapata thawabu yake.

Filipo akasema, “Ni Mwana wa Mungu.” Alipata thawabu Yake.

Chochote unachofikiria juu Yake, hiyo ni juu yako.

²¹⁹ Wewe unayelia hapo. Ulijua kuwa Kitu fulani kilikugusa, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mtu anayelia, aliyeketi papa hapa, hatufahamiani sisi kwa sisi. Sikujui. Lakini Mungu anakujua. Kama Mungu atanifunulia kilicho shida yako, utaamini kwa moyo wako wote? Kama utaamini, pungu mkono wako mbele na nyuma. Sawa.

²²⁰ Unasumbuliwa na tumbo. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu atakuponya? Vema, unaamini. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Je, kama ataniambia wewe ni nani, itakutia nguvu? Endelea kuinua mkono wako, ikiwa unaamini, upunge mbele na nyuma. Sawa. Itakuimarisha? Bw. Fred Moore. Hiyo ni kweli kabisa. Nenda nyumbani, bwana, kidonda hicho kwenye duodeni ya tumbo kimekuacha. Imesababisha hali ya fadhaa iliyofanya hivyo, lakini Yesu Kristo alikuponya alipokugusa pale.

²²¹ Mwanamke anayeketi karibu nawe hapo, loo, najua huyo ni nani. Ninamjua mwanamke huyo, ambaye jina lake ni...sijakosea. Ninaamini ni Bibi Greene, sivyo? Siwezi kukuita, Dada Greene, kwa sababu ninakujua. Lakini, hapa, ngoja kidogo. Hapana, sio kwa ajili yako. Unamuomba mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Na mtu huyo yuko katika

nchi kubwa mbali na hapa, ambapo kuna theluji nyingi inayoendelea. Ni Nebraska. Ni mwanamke aliye na kansa, ambaye unamwombea. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mtu aliye na kansa, ambaye unamwombea, huko Nebraska. Vema. Mungu akubariki.

Kuwa na imani! Amini!

²²² Mwanamke aliyeketi hapo, akifuta machozi kutoka kwa macho yake, yeye ni mgeni kwangu. Simjui mwanamke huyo. Huyo ni mume wake ameketi karibu naye; mtu huyo mkubwa. Huku hatufahamiani!

²²³ Unaamini kwamba Mungu husikia maombi? Unaamini ya kwamba huyu ni Roho wa Mungu, mama? Umetiwa uvuli wa mauti, sivyo? Ni kansa. Hatufahamiani. Iwapo hiyo ni kweli, pungu mkono wako kurudi nyuma. Hiyo ni kweli. Sijawahi kukuona, maishani mwangu. Wewe si wa jiji hili, unatoka ng'ambo ya mto mahali fulani. Hiyo ni kweli. Bibi Sanders ndilo jina. Hiyo ni kweli. Hilda ndilo jina la kwanza. Hiyo ni kweli kabisa. Simama kwa miguu yako, mama, na ukubali uponyaji wako kutoka kwa Yesu Kristo. Mungu akubariki. Unaona?

²²⁴ Mwamini Mungu. Usitie shaka. Wengine, ninyi nyote katika safu hizi hapa, mwaminini Bwana Yesu na mtapata afya.

²²⁵ Sasa, ni Yeye. Je, mnaamini kwamba ni Yeye? Unaona, sikujui. "Kama unaweza kuamini!" Ni juu yako.

²²⁶ Unaonekana unaomba, umeketi papa hapa, bwana. Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini ya kwamba ingekuwa ni Yeye? Mimi ni mgeni kwako. Wewe ni mgeni kwangu. Huu ni wakati wetu wa kukutana. Lakini Mungu anatujua sote wawili. Unaamini hilo? Mambo hayo ni kweli. Inua mkono wako. Unaamini kwamba unaenda nyumbani bila shida yako ya mgongo, Mungu atakuponya? Unaamini? Kurudi Ohio, Hamilton. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bw. Burkhart. Hiyo ni kweli. Yesu Kristo amekuponya sasa. Unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Amina. Mtu mwingine, amini.

²²⁷ Loo, unatambua Uwepo Wake? Je, unatambua kwamba Kitu fulani hakina budi kufanya hivyo? Hivyo ndivyo hasa Biblia ilivyosema Yeye alifanya kwanza, na kuahidi... Yeye alifanya jambo hilo mbele ya Myahudi, mbele ya Msamaria, na akaahidi kufanya jambo hilo mbele ya Mataifa. Hii ndiyo saa. Sio Mungu fulani wa kihistoria; bali Mungu Ambaye hutimiza ahadi Yake, anayeishi sasa hivi; Bwana Yesu, Yeye yule awaponyaye wagonjwa, jinsi vile vile alivyoifanya, njia ile ile, na kuiahidi katika siku za mwisho. Hii ni Krismasi tena, Nuru Yake iongozayo. "Unatazama nini, Ndugu Branham?" Ninamtaazama Yeye. Ni ulimwengu mwingine. Ni mwelekeo mwingine, ikiwa unataka kuuita hivyo. Ni katika ulimwengu wa roho.

²²⁸ Ninamwona mtu, mwenye moyo mzito sana, lakini namjua. Ndugu Funk, sikuijua mpaka sasa hivi. Uko kwenye shida.

Kivuli cheusi kabisa juu ya mama yako. Na unajua sijui hilo; ndiyo kwanza niingie. Lakini mama yako amefanyiwa upasuaji, akiwa hali mbaya, kansa. Una wasiwasi juu yake, na unaomba. Mungu aliyemrejesha baba yako katika akili yake timamu, akamrudishia afya yake, anaweza kumrejesha mama yako. Usiogope. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.”

²²⁹ Huyu hapo, juu ya mtu mwingine, lakini ninamjua. Lakini anamwombea mtu mwingine. Bibi Arganbright, kama utaamini, hiyo kansa itaponywa. Ni kwa ajili ya mtu mwingine. Amini.

²³⁰ Na wewe je? Unaamini, mama, kwamba mimi ni nabii Wake, mtumishi Wake? Unaugua kitu kile kile alichougua yule mwanamke, kutokwa na damu. Sawa. Wewe si wa mji huu. Unatoka Ohio, pia. Nawe ndiyo kwanza uponywe katika mmoja wa mikutano yangu, kitu fulani, wewe mwenyewe. Ulikuwa na kansa. Uлитиwa uvuli na mauti, na imetoweka sasa. Hiyo ni kweli. Ili uweze kujua kwamba mimi ni mtumishi Wake, kutokwa damu ni kutokana na umri wako. Lakini pia una baridi yabisi, au kama ugonjwa wa yabisi kavu, ni, unaposimama. Wewe hukakamaa asubuhi. Una shida na koo lako, pia. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake?

²³¹ Una mtu mwingine moyoni mwako, unayemwombea. Ni binti-mkwe wako. Ana ugonjwa wa kuvimba mishipa. Yeye ni mama wa kundi kubwa la watoto. Sivyo? Hiyo ni kweli kabisa. Jina lako ni Bibi Alice Thompson. Hiyo ni kweli kabisa. Rudi, pokea ulichoomba. Basi *yeye* ataponya, kwa sababu umemwamini Bwana Yesu. Sasa kama sisi ni wageni sisi kwa sisi, pungu, pungu mkono wako huku na huko, namna *hii*. Sikujui, sijui chochote kukuhusu.

²³² Ninaipa changamoto imani yako. Ninatoa changamoto kwa mtu yeyote hapa ndani, katika Jina la Yesu Kristo, kuamini katika Uwepo Wake. Sijali una shida gani, kama utaliamini.

²³³ Kumbukeni, hili ndilo jambo la mwisho atakalofanya kabla ya Kuja Kwake. Mnakumbuka aliyosema? “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma na Gomora, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwa Mwana wa Adamu.” Ujumbe ulikuwa nini?

²³⁴ Kulikuwa na Malaika watatu walioshuka. Wawili wao, Billy Graham na Jack Shuler walishuka wakaingia Sodoma, na kuhubiri tu ujumbe wa ukombozi wa Injili, kwa watu. Lakini Malaika mmoja alibaki nyuma na mteule, Ibrahimu na kundi lake.

²³⁵ Naye Malaika alikuwa amegeuza mgongo Wake kwenye hema. Na Sara akacheka, ndani ya hema. Naye Malaika akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Alijuaje kwamba alicheka, kwenye hema nyuma Yake? Huo ulikuwa ujumbe wa mwisho ambao Sodoma ilikuwa nao kabla ya maangamizi.

²³⁶ Na hizi hapa ishara za mwisho ambazo Mungu ataonyesha kabla ya maangamizi. Ipokee, iaini, na uoko.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

²³⁷ Je, unatambua Uwepo Wake? Je, unamtaka Yeye sasa, baada ya Yeye... unayo... Nimewahubiri ninyi Injili, nanyi mmesikia Ujumbe Wake. Ndipo mnamwona akishuka na kunena, Mwenyewe. Mwanadamu anaweza kusema chochote; lakini Mungu asiponena na kuthibitisha hilo, halifai chochote. Lakini Yeye ajapo, Mungu, na kuufanya Ujumbe kuwa halisi, na kuishi tena, basi ni Mungu. Je, unataka kumkubali sasa katika kujisalimisha kikamilifu kwa maisha yako? Naomba uinue mikono yako kwa muda mfupi tu, useme, "Nitainua mikono yangu. Sasa natoa yote yangu, yote yangu Kwake." Mungu akubariki. Mungu akubariki.

²³⁸ Wote wanaohitaji maombi, kwa ajili ya uponyaji, ninaamini ya kwamba kila mmoja wenu ataponywa. Hebu tuwaombe wagonjwa.

²³⁹ Bwana, ili mtu yeyote asiachwe nje, ili wote wapate! Tunajua, Bwana, kama mimi... simama hapa nikiwa dhaifu na nikitemeka, Wewe uko hapa. Imepita kivuli chochote cha shaka. Watu wanashangazwa na utisho wa Uwepo Mtakatifu wa Mungu, Krismasi nyingine, Nuru ile ile ya kimbinguni ikiangaza. Imeongoza wengi kutoka nyanja mbalimbali za maisha. Wamesikia Neno Lako likisomwa, na kuhubiriwa, na sasa wanakuona ukija na kulithibitisha Neno.

²⁴⁰ Biblia ilisema, "Wanafunzi walirudi na kuhubiri Neno kila mahali, Bwana akitenda kazi pamoja nao, akithibitisha Neno kwa ishara zilizowafuata," mambo ya mwisho yaliyoandikwa katika Maandiko, nje ya Ufunuo. Sasa tunaona tena. Kule Kuja kumekaribia, Bwana. Turehemu. Waponye wagonjwa wote walioko hapa asubuhi ya leo. Roho wako ni wa kweli. Ana nguvu, na Yuko hapa.

²⁴¹ Na kuna wengi hapa, Bwana, ambao ni watu wa maskani, ambao huja hapa. Umewarehemu, kuwaita.

²⁴² Na, hata hivyo, Bwana, Yuko juu ya wasikilizaji wote, sasa hivi. Ule Utukufu mkuu wa Shekina, Nguvu kuu za Kristo aliyefufuka, ule Upinde wa mvua wenye rangi nyingi, Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho, Nyota ya Asubuhi, Ua la Uwandani, yupo. Ponya, Bwana. Tunawatangaza kuwa wamepona, kwa neema Yako. Wape imani ya kuliaini, Bwana, na kulikubali sasa hivi, kwa utukufu wa Mungu. Jalia kila mgonjwa aponywe.

²⁴³ Na kila mtu ambaye amekosea, aliyeishi vibaya kwa mwenzi wake, jalia wasamehewe. Kila mtu anayevuta sigara au kunywa pombe, jalia wasamehewe. Jalia dhambi zao ziwe chini ya Damu, kwa Mungu aliyeko kila mahali Ambaye yuko hapa sasa; pengine

ndiyo karibu sana Naye waliowahi kuwa, katika maisha yao yote. Jalia sasa kwamba hii itapokelewa.

²⁴⁴ Utusikie, Bwana, Ee Mungu, Mfalme wetu mkuu, tunapoliitia Jina Lako, katika majira haya ya Krismasi; sio Baba Krismasi; bali Yesu aliyefufuka katika wafu, na yu hai, akijionyesha Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Ee Bwana, Wewe ndiwe Mungu, na Mungu pekee, na hakuna mwingine ila Wewe. Nasi tunakushukuru ya kwamba tuna majaliwa ya kuketi katika Uwepo Wake, katika mahali hapa padogo, panyenyekevu. Alijinyenyekeza Mwenyewe na kuja kati yetu. Tuna furaha sana kwa hili! Jina Lake takatifu lihimidiwe! Tunampa Yeye sifa, tangu asubuhi mpaka usiku, na kote katika nyakati za usiku, mioyo yetu inaimba nyimbo na sifa za Yehova. Shukrani ziwe Kwake, milele na milele!

²⁴⁵ Wachukue hawa, watoto Wako, Bwana, chini ya mbawa Zako, wafunike kama kuku afanyavyo vifaranga wake. Waongoze katika Maisha ya kilindi zaidi, na kwenye maisha ya furaha zaidi, na maisha yaliyokamilika zaidi, uwape ubatizo wa Roho Mtakatifu. Zifanye upya nafsi zao, Bwana, ziwe viumbe vipya katika Kristo, ili uweze kuishi na kukaa ndani yao, na kufanya kazi kupitia kwao, kama wanafunzi wako. Tujalie, Bwana. Kwa kuwa, tunaamini kwamba hivi karibuni mbingu itafunguka na Bwana wetu atakuja, nasi tutamwona Yeye tunayempenda. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili, kwa njia ya Yesu Bwana wetu.

²⁴⁶ Sasa tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, ninairudisha ibada kwa mchungaji.



YUKO WAPI, MFALME WA WAYAHUDI? SWA58-1221M

(Where Is He, King Of The Jews?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 21 Desemba, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org